



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

**TAARIFA YA UKAGUZI MAALUM KUHUSIANA NA MIAMALA  
ILIYOFANYIKA KATIKA AKAUNTI YA 'ESCROW' YA TEGETA, PAMOJA  
NA UMILIKI WA KAMPUNI YA IPTL**

---

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,  
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
Barabara ya Samora na Ohio,  
S.L.P. 9080,  
Simu: 255 (022) 2115157/8,  
Faksi: 255 (022) 2117527,  
Barua pepe: [ocag@nao.go.tz](mailto:ocag@nao.go.tz)  
Tovuti: [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz)  
**DAR ES SALAAM.**

Novemba, 2014

## **YALIYOMO**

### **Ukurasa**

<b>YALIYOMO</b>	i
<b>Vifupisho vya Maneno</b>	ii
<b>1.0 Utangulizi</b>	1
<b>SURA YA PILI</b>	6
<b>2.0 YALIYOJITOKESA KATIKA UKAGUZI MAALUM</b>	6
<b>SURA YA TATU</b>	53
<b>3.0 HITIMISHO</b>	53
<b>Viambatanisho</b>	54

## **Vifupisho vya Maneno**

BOT	Bank of Tanzania
BRELA	Business Registration and Licence Agency
BVI	British Virgin Islands (one of the British Overseas Territories)
COD	Commercial Operation Date
CRDB	Cooperative and Rural Development Bank
ICSID	International Center for Settlement of Investments Disputes
IPPA	Interim Power Purchase Agreement
IPTL	Independent Power Tanzania Limited
MW	MegaWatts
NBC	National Bank of Commerce
PAP	PanAfrica PowerSolutions Limited
PPA	Power Purchase Agreement
RITA	Registration, Insolvency and Trusteeship Agency
SCBHK	Standard Chartered Bank Hong Kong
Sh.	Shilingi - Fedha za Kitanzania
TANESCO	Tanzania ElectricitySuppliesLimited
TISS	Tanzania Inter Banks Settlement system
TRA	Tanzania Revenue Authority
TT	Telegraphic Transfer
TZS	Tanzanian Shillings
USD	United United States Dollars
VAT	Value Added Tax
VIP	VIP Engineering and Marketing

Mh.Waziri Mkuu,  
Ofisi ya Waziri Mkuu,  
S.L.P 980,  
DODOMA.

**TAARIFA YA UKAGUZI MAALUM KUHUSIANA NA MIAMALA ILIYOFANYIKA  
KATIKA AKAUNTI YA ‘ESCROW’ YA TEGETA PAMOJA NA UMILIKI WA KAMPUNI  
YA IPTL**

**SURA YA KWANZA**

**1.0 Utangulizi**

Tumekamilisha ukaguzi maalumwa akaunti ya Escrow ya Tegeta iliyokuwa katika Benki Kuu ya Tanzania, Utekelezaji wa Mkataba wa Ununuzi wa Umeme na Umiliki wa Kampuni ya Independent Power Tanzania Limited(IPTL).

**1.1 Chimbuko la Ukaguzi**

Ukaguzi huu umetokana na barua yenyewe Kumb. Na PM/P/1/567/62 ya tarehe 10 Juni 2014 kutoka kwa Mh. Waziri Mkuu. Kabla ya barua hii, ukaguzi huu ulikwishaombwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kupitia barua Na. CBD.88/417/01/40 ya tarehe 12 Machi 2014 na Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia barua Na. CBC.155/188/01/31 ya tarehe 20 Machi 2014. Barua ya Mh. Waziri Mkuu imefanya rejea katika maombi yaliyotangulia kutoka kwa Katibu wa Bunge na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliwasiliana na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini na Katibu wa Bungekupitia barua Na. CA.27/442/01/53 ya tarehe 17 Aprili, 2014 ili kukubaliana juu ya hadidu za rejea zitakazoongoza ukaguzi huu. Hadidu za rejea husika ziliridhiwa na taasisi hizo mbili kupitia barua Na. CBD.88/417/01/11 ya tarehe 5 Mei 2014kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini na barua Na. CBC.155/188/01 ya tarehe 03/05/2014kutoka kwa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (**Kielelezo 1**).

**1.2 Historia ya Uanzishwaji na Umiliki wa Kampuni ya IPTL na Suala la Akaunti ya Escrow ya Tegeta**

Mwaka 1995, Serikali kupitia TANESCO iliingia mkataba na Kampuni ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL) kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kufua umeme wenye uwezo wa kuzalisha Megawati 100(**Kielelezo 2**). Kampuni ya IPTL ilikuwa inamiliikiwa na kampuni ya VIP Engineering and Marketing Ltd ya Tanzania kwa 30% na Mechmar Corporation (MECHMAR) ya Malaysia kwa 70%. Mkataba huu ulihusu IPTL kuzalisha umeme na kuiuzia TANESCO (**Kielelezo 3**).

Katika kipindi cha kutekeleza mradi huu, TANESCO iligundua kuwa Kampuni ya IPTL ilikuwa ikiilipisha tozo kubwa yagharama za uwekezaji(capacity charges) ambapo tarehe 17 June, 2004 ilitoa notisi ya kupinga ankara za madai kutoka IPTL.TANESCO ilidai kukotolewa upya kwa viwango(tariffs) vinavyolingana na kiwango cha mtaji (equity) ambacho IPTL inaonesha kwenye vitabu vyta hesabu na kwa Msajili wa Makampuni (BRELA) cha Shilingi 50,000 badala ya Dola za Kimarekani 38 Milioni(**Kielelezo 4 na 5**).

Kutokana na kutoridhika kwa TANESCO na viwango vyta tozo vilivyokuwa vinatumwa na ITPL, TANESCO ilisitisha kumlipa IPTL malipo ya ‘capacity charges’ badala yake tarehe 5 Julai, 2006 mkataba wa akaunti ya Escrow ulisainiwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya IPTL wakati Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa Wakala wa utekelezaji wa mkataba huo kwa mujibu wa Kipengele Na.6.8 (b) cha Mkataba wa Kununua Umeme (PPA) ambapo fedha zote za ‘capacity charges’ ziliwu zikilipwa katika akaunti hiyo(**Kielelezo 6 na Rejea Kielelezo 2**).

Tarehe 5 Septemba 2013 Mahakama Kuu ya Tanzania iliridhia kuondolewa kwa shauri Na. 49 la 2002 na Na.254 la 2003 (chini ya Mheshimiwa Jaji Utamwa)kuhusiana namaombi ya ufilisi wa IPTL yaliyofunguliwa na VIP Engineering and Marketing. Katika uondoshwaji wa shauri hilo Mahakama Kuu ya Tanzania ilikabidhi masuala yote yahusuyo IPTL ikiwemo mtambo uliopo Tegeta kwa kampuni ya Pan Africa Power Solutions(PAP) ambayo baadaye ilileta madai ya kulipwa fedha zilizokuwemo katika akaunti ya escrow ya Tegetailiyokuwepo Benki Kuu ya Tanzania(**Kielelezo 7**).

Baada ya mashauriano kati ya TANESCO, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, Benki Kuu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hatimaye mwezi Desemba, 2013 PAP ililipwa fedha zilizokuwepo katika ya Escrow ya Tegeta iliyokuwa Benki Kuu ya Tanzania.

### **1.3 Mamlaka ya Ukaguzi**

Kulingana na Ibara ya 143 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaruhusiwa kisheria kufanya ukaguzi maalum katika taasisi zote za umma.

### **1.4 Madhumuni na Wigo wa Ukaguzi Huu**

Madhumuni ya kufanya ukaguzi huu maalumu ni kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa mapendekezo yake kuhusiana

na utaratibu uliotumika kutoa fedha kutoka akaunti ya Escrow ya Tegeta iliyokuwa katika Benki Kuu ya Tanzania.

Ukaguzi huu maalum umefanyika kwa kuzingatia matakwa ya viwango vya kimataifa vya ukaguzi na kuzingatia hadidu za rejea kama ziliivyordhiwa na pande zote. Hata hivyo ukaguzi huu hautoi maoni ya ukaguzi (audit opinion) badala yake unatoa mapendekezoyanayolenga katika kushughulikia mapungufu yaliyobainika katika ukaguzi huu.

Ingawa matokeo ya ukaguzi huu yanajumuisha uchambuzi wa masuala ya kisheria, ukaguzi huu hautoi maoni juu ya kuwa au kutokuwa na hatia kwa mtu, chombo au taasisi yoyote iliyohusika katika ukaguzi huu.

Ukaguzi huu ulijikita katikauchambuzi wa nyaraka, taarifa na kumbukumbu kama tulivyozipokea kutoka katika taasisi husika ikiwa ni pamoja na kufanya mahojiano na wahusika mbalimbali katika suala la malipo yaliyofanyika kutoka katikaakaunti ya Escrow ya Tegeta, umiliki wa IPTL na utekelezaji wa mkataba wa ununuzi wa umeme toka IPTL. Endapo nyaraka, taarifa ama kumbukumbu nyingine zitapatikana vinaweza kubadili mwelekeo wa maoni na hitimisho la ukaguzi huu.

### **1.5 Hadidu za Rejea**

Ukaguzi maalumu ulifanyika kwa kuzingatia hadidu za rejea kama zilivyoorodheshwa hapa chini:

- i. Kuchunguza utekelezajiwa Mkataba wa Kuzalisha Umeme kati ya kampuni ya IPTL na TANESCO,
- ii. Kufanya uchunguzi iwapo BoT imetimiza wajibu wake, na kuchukua tahadhari ya kutosha kabla ya kuhamisha fedha taslimu Dola za Kimarekani 22,198,544.60 na Sh.8,020,522,330.37 na Hati Fungani zenye thamani ya Sh.153,369,164,254.97 kutoka ‘Escrow Account’ iliyoko Benki Kuu ya Tanzania kwenda IPTL,
- iii. Kuchunguza sababu za kufungua akaunti maalum (Escrow Account) na pia chanzo cha mgogoro kuhusu tozo kati ya TANESCO na IPTL na kuthibitisha kuwa mgogoro uliamuliwa kwa faida ya pande zote mbili yaani Serikali (TANESCO) na IPTL. Hii itahusisha kuchunguza na kubainisha wahusika katika mapungufu yatakayokuwa yamebainika kuhusu suala la IPTL,
- iv. Kuchunguza kama wakati akaunti maalumu ya BoT (Escrow account) inafunguliwa Kampuni ya Mechmar ilikuwa inamiliki IPTL. Pia, Kuthibitisha kwamba kampuni ya Mechmar ilikuwa imehamishia umiliki wake kwa kampuni ya Pan Africa Power Solutions (T) Limited (PAP) kabla ya kafilisiwa.

- v. Kuthibitisha kama Kampuni ya PAP imenunua hisa zote za Kampuni ya Mechmar katika IPTL na sasa inamiliki IPTL,
- vi. Kuchunguza kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisamehe kodi ya VAT ya jumla ya bilioni Sh.26 kutokana na tozo ya “capacity charge”; ikiwa ni pamoja na usahihi wa mamlaka yake kisheria,
- vii. Kuchunguza kiwango cha fedha kilichopaswa kuwepo kwenye Akaunti maalum ya BoT “Escrow Account”, kiwango cha fedha kilichokuwepo kwenye akaunti hiyo wakati BOT inahamisha fedha zilizokuwepo kwenye akaunti ‘Escrow Account’ kwenda IPTL na kiwango cha fedha kilichopaswa kulipwa zaidi kutoka TANESCO kwenda IPTL.Hii itahusisha pia kuchunguza na kutoa taarifa kuhusu kiasi cha fedha kilichowekwa na kila mhusika hadi uamuji wa Mahakama Kuu ya Tanzania kuhusu kesi ulipotolewa,
- viii. Kuchunguza madai ya Benki ya Standard Chartered (Hong Kong) kwa IPTL na madai mengine yoyote yanayohusiana na Mkataba wa kuzalisha Umeme wa IPTL na iwapo Serikali imejihadhari na uwezekano wa madai yanayoweza kufunguliwa dhidi yake na wadai mbalimbali,
- ix. Kuchunguza iwapo Wizara ya Nishati na Madini ambayo iliingia Mkataba na IPTL wa kufungua akaunti maalum ya Escrow ilifanya uadilifu na kuweka uangalifu wa kutosha kabla ya kuingia makubaliano na IPTL ya kutoa fedha zilizokuwepo kwenye akaunti hiyo na kuilipa IPTL.
- x. Kufanya uchunguzi kuhusu hisa za Kampuni ya Mechmar inayosemekana kafilisika na iliyokuwa na hisa nyingi IPTL kwamba sasa hisa hizo zinamiliikiwa na Kampuni ya Pan Africa Power Solutions (T) Limited (PAP).
- xi. Kufanya uhakiki wa hatua zilizofuatwa tangu kesi ilipofunguliwa hadi uamuji wa Mahakama ulipotolewa. Kiasi kilichokwuwa katika akaunti baada ya uamuji wa Mahakama Kuu na kulingana na mkataba,
- xii. Kutoa mapendeleko ya njia sahihi za kisheria zinazoweza kutumika kwa ajili ya kulinda serikali isipate hasara zaidi katika utekelezaji wa mkataba wa uzalishaji umeme kati ya TANESCO na IPTL chini ya wamiliki wapya wa IPTL yaani PAP,
- xiii. Kutoa mapendeleko juu ya hatua ambazo zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya wahusika kulingana na matokeo ya ukaguzi maalum.  
**(Rejea Kielelezo 1).**

## **1.6 Njia Zilizotumika Katika Ukaguzi**

Timu ya ukaguzi maalum ilitumia njia mbalimbali katika kupata taarifa na ushahidi katika kukamilisha ukaguzi huu. Njia zilizotumika ni pamoja na kuitia nyaraka, mikataba, majalada, taarifa kuhusiana namashauri mbalimbali kutoka watu, taasisi binafsi na za umma. Baadhi ya taasisi hizo ni TANESCO, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Benki Kuu ya Tanzania, Benki ya Stanbic, Benki ya Mkombozi, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)na Mahakama ya Tanzania.

Ukaguzi pia ulihakiki na kuthibitisha masuala mbalimbali katika nchi za Malaysia, British Virgins Islands (BVI) na China (Hong Kong) ambapo mahojiano yalifanyika na kupata taarifa kutoka kwa wahusika katika suala hili wakiwemo; Wafilisi wa Mechmar, Standard Chartered Bankpamoja na Mahakama Kuu za Malaysia na BVI.

Vile vile timu ilifanya mahojiano na baadhi ya waheshimiwa Wabunge, Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na watu mbalimbali kama orodha iliyoambatishwa katika taarifa hii (**Kiambatanisho Na. 1**).

## **1.7 Matumizi ya TaarifaHii**

Taarifa hii ni kwa ajili ya matumizi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ndiyo waliomba kufanyika kwa ukaguzi huu maalum.

Taarifa hii yaweza kutumika kama ushahidi katika mashauri ya madai au jinai. Pia taarifa hii yaweza kutumiwa na Mamlaka, taasisi za Serikali au vyombo vyta kusimamia utekelezaji wa sheria kwa ajili ya kuchukua hatua stahikipale itakapotakiwa kufanya hivyo.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi haitahusika na matumizi ya taarifa hii na chombo, taasisi au mtu mwingine zaidi ya vyombo au taasisi zilizotajwa hapo juu.

## SURA YA PILI

### 2.0 YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI MAALUM

#### 2.1 HADIDU REJEA NA. 1

**Kuchunguza Utekelezaji wa Mkataba wa Kuzalisha Umeme Kati ya Kampuni ya IPTL na TANESCO**

##### 2.1.1 Mradiwa Kufua Umeme wa Kampuni ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL)

Katika miaka ya 1990, Tanzania ilikuwa ikitabiliwa na tatizo la uhaba wa maji katika mabwawa ya kuzalisha umeme hali iliyopelekea kuwepo kwa upungufu wa umeme na kuathiri shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Kwa wakati huo, TANESCO pekee ndiyo iliyokuwa na jukumu la kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme. Mwaka 1992 Serikali ilipitisha Sera ya Nishati (Energy Policy) iliyoruhusu uwekezaji binafsi katika sekta ya nishati. Katika kutekeleza sera hiyona kuchukua hatua za dharura, Serikali ilialika wawekezaji binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa umeme (**Kielelezo 8**).

Wizara ya Maji Nishati na Madini iliingia katika Memoranda ya Makubaliano (MoU) na Kampuni ya Mechmar ili kuleta suluhisho la kukabiliana na upungufu wa umeme. Kwa mujibu wa Kipengele cha 5 cha MoU, hitaji kubwa la TANESCO ilikuwa ufumbuzi wa haraka. Hata hivyo tangu kuingiwa kwa makubaliano husika tarehe 27 Agosti 1994 mtambo wa umeme ulikamilika kwa ajili ya uzalishaji mwaka 1998 ingawa umeme ulianza kuzalishwa na kuuzwa tarehe 15 Januari 2012.

Pia, Kipengele cha 4 cha MoU kinaekeleza muda wa mradi kuwa miaka 15, hata hivyo mkataba uliosainiwa ulikuwa wa miaka 20 (kipengele Na.2.1 cha PPA) (**Kielelezo 10 na Rejea Kielelezo 2**).

Mwaka 1994 Kampuni ya IPTL ilianzishwa chini ya umiliki wa Kampuni ya Mechmar kutoka Malaysia na Kampuni ya VIP Engineering and Marketing (VIP) ya Tanzania. Kampuni ya MECHMAR ilimiliki asilimia 70 na VIP asilimia 30 ya hisa za IPTL (**Rejea Kielelezo 3**). Mwaka 1995 Serikali ilingia mkataba wa kununua umeme wa Megawati (MW) 100 kutoka kampuni ya IPTL (**Rejea Kielelezo 2**).

Kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa na Serikali ya Tanzania katika ICSID kuhusu Shauri Na. ARB/98/8, tarehe 3 Mei 1995 rasimu ya mkataba wa IPTL ilijadiliwa na Baraza la Mawaziri, ambapo ilielekezwa kuwa Kamati ya Uchumi na Fedha ya Baraza la Mawaziri ikutane na kujadili viwango kuhusiana na gharama za uzalishaji, gharama za umeme, uwezo na matumizi ya mitambo na kisha kumshauri Mh. Rais wa Tanzania

kwamba Serikali iridhie kuingia Mkataba wa Kununua Umeme (PPA). Pia TANESCO waruhusiwe kuingiamkataba huu na IPTL, kadhalika Wizara ya Maji, Nishati na Madini iingie Makubaliano ya Utekelezaji wa Mkataba huu. Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara, ilifahamika kuwa Mh. Rais alikubaliana na mapendekezo ya Baraza la Mawaziri (Para 21 ya ICSID 1 ARB/98/8) (Kielelezo 11).

### **2.1.2 Mikataba Inayohusiana na Utekelezaji wa Mradi wa Uzalishaji wa Umeme wa IPTL**

Katika kutekeleza mradi wa uzalishajiumemewa MW 100, Wizara ya Maji, Nishati na Madini, TANESCO na IPTL ziliingia mikataba mbalimbali kama inavyoonekana katika Jedwali T1:

**Jedwali T1: Mikataba iliyoingiwa katika utekelezaji wa mradi**

S/N	Mkataba	Tarehe	Muda	Dhima ya Mkataba
1	Mkataba wa KununuaUmeme (Power Purchase Agreement- (PPA)) baina ya IPTL na TANESCO	26 Mei 1995	Miaka 20 kuanzia siku ya kuanza uzalishaji (COD) tarehe 15 Januari, 2002	Uzalishajina ununuzi wa MW 100 kati ya IPTL na TANESCO
2	Mkataba wa Utekelezaji wa Mradi wa Kufua Umeme Megawati 100 (Implementation Agrement) baina ya Serikali na IPTL	8 Juni, 1995	Uhai wa Mkataba huu unategemea uhai wa Power Purchase Agreement (Ibara iii)	Kuhakikisha mradi wa kuzalisha umeme kati ya TANESCO na IPTL unatekelezeka Pia kuhakikisha taratibu za ujenzi, uendeshaji, upatikanaji na uwezeshaji wa mradi unaendana na sera ya nchi. Kuhakikisha upatikanaji wa vibali vyote vya kiserikali
3	Mkataba wa Dhamana (A Guarantee Agreement) baina ya Serikali na IPTL	8 Juni, 1995	Uhai wa Mkataba huu unategemea / unaendana na uhai wa 'Power	Kuidhamini TANESCO katika ulipajiwani 'capacity charges' na 'energy charge'

			Purchase Agreement' (Article I na III)	
4	Mkataba wa nyongeza kwa (Power Purchase Agreement- Addendum No. 1) to the Power Purchase Agreement)	9Juni, 1995	Nyongeza ya 'Power Purchase Agreement' kw a kipindi chote cha PPA	Kuelekeza ukokotoaji wa viwango vya tozo (tariffs) ya 'capacity charges' Kuainisha washirika katika Makubaliano ya 'Escrow'

**(Kielelezo 12na 13 na Rejea Kielelezo 2)**

Mwaka 1998 TANESCO ilifungua shauri dhidi ya IPTL Na. ARB/98/8 katika Baraza la Kimataifa la Usuluhihi wa Migogoro ya Uwekezaji (International Centre for Settlement of Investment Disputes-ICSID) ikidai kusitishwa kwa PPA kutokana na ukiukwaji wa baadhi ya vipengele katika utekelezaji wake.

Kutokana na shauri hilo, Mkataba wa uzalishaji umeme pamoja na kwamba uliingiwa mwaka 1995 na ujenzi wa mitambo kukamilika mwaka 1997, uzalishaji wa umeme ulianza Januari 15, 2002 (commercial operation date). Hivyo kwa kuwa mkataba ni wa miaka 20 unategemewa kuisha mwaka 2022.

Vile vile uliibuka mgogoro mwingine ambapo mwezi Juni, 2004 TANESCO ilianza kupinga ankara za madai ya 'capacity charges' za IPTL zilizokuwa zinatozwa. Kwa mujibu wa Kipengele Na. 6.8 (a) cha PPA, TANESCO ilitoa pingamizi hizo kwa kutoa 'Invoice Dispute Notices' kwa madai kuwa ililipishwa 'tariff' kubwa zaidi isivyostahili.

IPTL iliwasilisha maombi ya kutafsiriwa kwa 'ICSID 1 Award' ilipofika Juni 2008 baada ya TANESCO kutolipa 'capacity charges' licha ya IPTL kuzalisha umeme katika vipindi tofauti. Shauri hili lilisitishwa na 'ICSID' kwa mujibu wa sheria Na. 44 ya sheria za ICSID (**Kielelezo 14 Kesi ya ICSID Na. ARB/10/20 Para 46-48**).

Tarehe 15Septemba 2010 SCBHK ilipeleka 'ICSID' maombi ya kutolewa tamko la kuidai kwa TANESCO, ambapo ICSID ilitoa uamuzi wa awali mwezi Februari 2014 (ICSID 2) uliojumuisha pamoja na mambo mengine ni kwambakiwango cha tozo ya gharama za uwekezaji zinapaswa kukokotolewa upya ili kuonyesha kwamba mtaji (equity contribution) wa IPTL ultokana na mkopo wa wanahisa (shareholders loan) na siyo mtaji wa wanahisa uliolipiwa (paid up share capital)(**Rejea Kielelezo 14**).

### **2.1.3 Masuala yaliyojitokeza katika uhakiki waMkataba**

Baada ya kufanya mahojiano na Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO Mhandisi Felchesmi Mramba, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Bw. Eliakim Maswi na baadhi ya watendaji husika wa TANESCO na Wizara, maafisa wa IPTL na kuhakiki mikataba iliyoingiwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ufuaji Umeme wa Megawati 100, timu ya ukaguzi ilibaini yafuatayo:

**(i) Kutofanyika kwa uchambuzi wa vihatarishi (Risk analysis)**

Ukaguzi huu maalum umebaini kuwa, mkataba wa Kuzalisha Umeme kati ya Kampuni ya IPTL na TANESCO ulikuwa na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikiathiri utekelezaji wake. Katika ukaguzi huu, hatukupata ushahidi kuwa TANESCO walifanya uchambuzi wa vihatarishi ambavyo vingeweza kuliathiri Shirika wakati wa utekelezaji wa mkataba huu.

**(ii) Kutokubaliana kwa gharama za uwekezwaji wa mradi wa IPTL**

Baada ya ujenzi wa mradi, TANESCO ilibaini kuwa gharama zilizoonyeshwa kwa ajili ujenzi wa mradi kuwa juu isivyostahili. Ambapo miongoni mwa masuala yaliyopelekea kuamini kuwa gharama za mradi zimekuzwa ni kufungwa kwa injini za ‘medium speed’ badala ya ‘slow speed’.

Kwa mujibu wasehemu ya awali (Recital) ya PPA, injini za mtambo wa kufua umeme zilizokuwa zinahitajika ni za mwendokasi mdogo(Slow Speed)badala yake IPTL walismikia mitambo yenyenye mwendokasi wa kati(Medium Speed) ambazo gharama zake zilikuwa ndogo. Hivyo TANESCO ilidai kuwa gharama za uwekezaji zilizoonyeshwa zipunguzwe.

Suala hilolilipelekwa ‘ICSID’ambako iliamuliwa gharama za uwekezaji kupunguzwa kutoka USD 163.531 hadi 127.201Milioni, hivyo kusababisha ‘capacity charges’ kupungua kutoka US\$.3.6Milioni hadi US\$.2.6Milioni kwa mwezi.

**(iii) Kutoanzishwa kwa Kamati ya Uendeshaji (Operations Committee)**

Kwa mujibu wa Kifungu Na 8.3 (a) cha PPA, TANESCO na IPTL katika mkatabahuo walipaswa kuunda Kamati ya Uendeshaji wakati ama kabla ya kipindi cha siku 180 kabla ya siku ya kuanza uzalishaji (Commercial Operation Date). Kamati hiyo ilitakiwa kuwa na wajumbe 6 ambapo kila upande wa mkataba ungewakilishwa na wajumbe watatu.

Kamati hii ilitakiwa kuratibu uendeshaji wa mtambo (facility) kwa mujibu wa taratibu za uendeshaji kulingana na Kipengele Na 7.4 cha PPA. Pia Ibara ya XVII inaelezea kuwa kamati hiyo ingehusika na

usuluhishi wa migogoro ambayo inaweza kutokea katika kutekeleza mkataba wa kuzalisha umeme.

Kwa mujibu wa Kipengele Na 18.1 cha PPA, pale ambapo mgogoro unapotokea Kamati ya Uendeshaji inawajibu wa kupitia mgogoro husika, kusuluhisha, kutoa mapendekezo yanayopaswa kufanyiwa kazi katika muda wa siku thelathini (30). Endapo mgogoro husika hautamalizika katika ngazi ya kamati hii, basi utapelekwa kwa wakuu wa taasisi. Hadi wakati wa ukaguzi huu mwezi Oktoba 2014, kamati hii haikuwa imeanzishwakinyume na utaratibu ulioainishwa katika PPA.

#### **Mapendekezo**

- i. Menejimenti ya TANESCO ifanye uchambuzi wa vihatarishi vinavyoweza kuiathiri katika utekelezaji wa PPA.
- ii. Kwa kuwa mkataba wa ununuzi wa umeme bado unaendelea kati ya TANESCO na IPTL, pande hizo zinapaswa kuanzisha kamati ya uendeshaji kulingana na matakwa ya mkataba.
- iii. TANESCO ifuutilie utekelezaji wa maamuzi ya awali ya Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji (ICSID) dhidi ya Shauri Na. ARB/10/20 (ICSID 2) pamoja na mambo mengine ni kuhusu kukokotolewa upya kwa gharama za uwekezaji.

## **2.2 HADIDU YA REJEA NA.2**

Kufanya uchunguzi iwapo BoT imetimiza wajibu wake na kuchukua tahadhari ya kutosha kabla ya kuhamisha fedha taslimu Dola za Kimarekani 22,198,544.60 na Shilingi 8,020,522,330.37 pamoja na Hati Fungani zenyenye thamani ya Shilingi 153,369,164,254.97 kutoka Escrow Account iliyoko Benki Kuu ya Tanzania kwenda IPTL

Timu ya ukaguzi ilipitia nyaraka mbalimbali ili kuhakiki iwapo Benki Kuu ilitimiza wajibu wake na kuchukua tahadhari kabla ya kuhamisha fedha kutoka katika akaunti ya Escrow. Pia timu ilipata maelezo toka kwa Gavana wa Benki Kuu Prof. Beno Ndulu, Mwanasheria wa Benki Kuu Mustapha Ismail (Associate Director Litigation & Investigation) na Bw. V. Msaki (Advisor, Foreign Payments and Settlements).

### **2.2.1 Majukumu na wajibu wa Benki Kuu Katika Akaunti ya Escrow**

Kwa mujibu wa kipengele Na.1.1 na Na 7.1 cha Makubaliano ya Escrow Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ilikubali kuwa wakala wa akaunti ya Escrow ambayo ilifunguliwa kufuatia makubaliano baina ya Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Nishati na Madini na Kampuni ya IPTL yaliyofikiwa tarehe 5 Julai, 2006 (**Rejea Kielelezo 6**).

Kipengele Na. 2.1 cha Makubaliano ya Escrow kimeainisha kuwa wakala wa Escrow (BoT) ana jukumu la kufungua na kuhifadhi akaunti ya Escrow katika sarafu mbili (Shilingi za Kitanzania na Dola za Kimarekani). Vile vile Kipengele Na.7 cha Makubaliano hayo kimeainisha majukumu ya Wakala (BoT) kuwa ni pamoja na kupokea, kuhifadhi na kuwekeza fedha za akaunti ya Escrow na kutolewa kwa fedha hizo kwa mujibu wa taratibu zinazolezwa katika sehemu ya nne IV ya Makubaliano hayo.

Kipengele Na 4.1 cha Makubaliano ya Escrow kinaipa mamlaka Benki Kuu kuwa mtoaji pekee wa fedha katika akaunti hiyo. Kadhalika Benki Kuu iliwajibika kutoa taarifa kila robo mwaka kwa pande zote za makubaliano kuhusiana na hali ya akaunti katika kipindi husika kama ilivyoanishwa katika Kipengele Na.5.3 na 5.4 cha Makubaliano ya Escrow.

Kipengele Na. 7.7 cha Makubaliano ya Escrow kinaeleza kuwa iwapo wakala wa Akaunti ya Escrow kwa nia njema asipokuwa na uhakika kuhusu upande unaostahili kulipwa fedha kutoka kwenye Akaunti ya Escrow kutokana na mgogoro baina ya pande hizo, atasubiri hukumu ya mwisho ya msuluhishi itakayomuelekeza upande stahili wa kulipwa fedha hizo ama makubaliano ya kimaandishi baina ya pande husika.

Hadi kufikia tarehe 22 Novemba, 2013 akaunti ya Escrow ilikuwa na kiasi cha dola za kimarekani 22,198,544.60, shilingi za kitanzania 8,020,522,330.37 na hati fungani za siku 182 za Sh.159,231,370,000 (thamani Sh.148,071,081,052 na riba ya Sh.11,160,288,948) (**Kielelezo**

15). Ambapo pia ukaguzi ulibaini kuwa kiasi cha hati fungani kilichoainishwa katika hadidu ya rejea cha Sh.153,369,164,254.97 kinatofautiana na kiasi halisi kilichobainika cha Sh. 159,231,370,000.

Baada ya hukumu ya Septemba 5, 2013 ya Mahakama Kuu ya Tanzania juu ya Shauri la Madai Na.49 la 2002, BoT ilipokea nakala mbalimbali za mawasiliiano kati ya Wizara ya Nishati na Madini, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kampuni ya IPTL na TANESCO yaliyobainisha nia ya kutolewa kwa fedha kwenye akaunti ya Escrow (**Kielelezo 16, 17 na 18**).

Tarehe 23 Septemba, 2013 Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliakim Maswi kupitia barua Kumb. Na. CDB.88/417/31 kwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Dr. S. Likwelile aliiitisha kikao cha dharura cha wadau husika siku ya tarehe 24 septemba, 2014 kujadili makubaliano yaliyofikiwa juu ya kuhamisha fedha kutoka katika akaunti ya Escrow (**Rejea Kielelezo 18**).

Katika kikao hicho cha dharura cha tarehe 24 Septemba, 2014 ambacho kilihudhuriwa na wawakilishi kutoka Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na TANESCO, BoT iliwaeleza wawakilishi hao utaratibu uliopaswa kufuatwa na mambo ya kuzingatiwa ili kutoa fedha katika akaunti ya Escrow. Pia BoT iliwataka wadau hao kuhakikisha tahadhari za kutosha zinachukuliwa kabla ya kutoa fedha katika akaunti hiyo (**Rejea Kielelezo 18**).

Pia kikao hicho kiliazimia kuundwa kwa timu ndogo ya wataalamu kutoka Benki Kuu, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, TANESCO na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kutathmini athari zinazoweza kujitokezaiwapo fedha hizo zingetolewa. Timu ilipaswa kutoa taarifa yake kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kabla ya tarehe 27 Septemba 2014 (**Kielelezo 19**).

Taarifa ya Kamati ilikabidhiwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Dr. S. Likwelile ambaye pia aliiwasilisha kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini Bw. Eliakim Maswi kupitia barua Kumb Na. CAC/184/211/01/23 ya tarehe 30 Septemba, 2013 (**Rejea Kielelezo 19**). Kupitia kipengele Na.7.1 hadi Na.7.3 cha taarifa, Kamati ilipendekeza kuwa:

- (i) Tanesco na IPTL wanapaswa kukamilisha uhakiki wa madai ya ‘capacity charges’ na kuwasilisha makubaliano kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini,
- (ii) IPTL itoe kinga kwa Serikali, Wizara ya Nishati na Madini na TANESCO dhidi ya madai yoyote yanayoweza kutokea baada ya utolewaji wa fedha katika akaunti ya Escrow,

- (iii) Mkataba wa ufuaji wa umeme urejewe upya ili kuweza kuingiza ‘commitment’ ya Kampuni ya PAP kulingana na hukumu ya Mahakama Kuu ya Tanzania.

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Dr. Servacius Likwelile alibainisha kuitia barua Kumb Na. CAC/184/211/01/23 ya tarehe 30 Septemba 2013 alipowasilisha taarifa ya kamati ya wataalam kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini (nakala kwa Gavana na Mwanasheria Mkuu), kuwa alikusudia wadau husika kukutana na kujadili taarifa ya kamati ili kufikiwa kwa maamuzi stahiki.

Baada ya kupokea nakala ya barua Na. CAC/184/211/01/23 ya tarehe 30 Septemba 2013 ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Dr. Servacius Likwelile, Mwanasheria Mkuuwa SerikaliMh. Jaji Fredrick Werema kuitia barua Kumb. Na. AGCC/E.80/6/65 ya tarehe 2 Oktoba, 2013 alimuarifu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dr. Servacius Likwelile kuwa ameipitia ripoti husika na kwamba jambo pekee linaloweza kuleta tatizo ni kuhusu fedha ziliwekezwa na Benki Kuu katika hati fungani (**Kielelezo 20**).

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alishauri kuwa fedha hizo zilipwe kwa IPTL ili jambo hilo lifungwe na kuiwezesha Serikali kujiepusha na mashauri yasiyo na tija kwake, na kusisitiza kuwa uamuvi wowote wa kutoa fedha kwenye akaunti ya Escrow unalindwa na hukumu ya Mahakama Kuu ya Tanzania (Mh. Jaji Utamwa) ya tarehe 5 Septemba, 2013 (**Rejea Kielelezo 20**).

Makubaliano ya kutolewa kwa fedha baina ya Wizara ya Nishati na Madini yalifanyika kwa mujibu wa Kipengele Na. 7.7(ii) cha makubaliano ya Escrow, ambayo yaliruhusu BoT (wakala wa akaunti ya Escrow) kuilipa IPTL fedha husika (**Kielelezo 21**).

## **2.2.2 Hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu Kabla ya Kuhamisha Fedha Kutoka Kwenye Akaunti ya Escrow**

Kwa mujibu wa Mwanasheria wa Benki Kuu Bw M. K. Ismail, Benki Kuu ilishiriki katika kikao kilichoitishwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini kuitia barua Kumb. Na. CDB.88/417/31 na kufanyika tarehe 24, Oktoba 2013(**Rejea Kielelezo 18**). Kikao kulihudhuriwa na washiriki kutoka Benki Kuu, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na TANESCO, BoT iliishauri Serikali kujiridhisha zaidi kabla ya kutoa fedha kwenye akaunti ya Escrow juu yamambo yafuatayo:

- i. Kuwepo na ushahidi unaoonesha kuwa hisa zilizokuwa zinamilikiwa na Mechmar zimenunuliwa na PAP na manunuvi husika kusajiliwa BRELA;

- ii. Kuwepo na ushahidi kuwa mgogoro uliokuwepo baina ya IPTL na TANESCO kuhusiana na “capacity charges” umepatiwa suluhu, na imeafikiwa kuwa IPTL ilipwe fedha husika;
- iii. Kupata ushauri kutoka Wizara ya Fedha juu ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), ambapo Tarehe 15 Novemba, 2013 kuitia barua Kumb. Na. NC.53/135/068 kwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Gavana wa Benki Kuu Prof Benno Ndulu iliomba muongozo juu ya madai ya TRA kuhusu VAT kabla ya kutoa fedha kwenye akaunti ya Escrow.
- iv. Gavana wa Benki Kuu, Prof. Beno Ndulu kuitia barua Kumb. Na. AC.53/195/01 tarehe 24 Oktoba, 2013 kwenda kwa Katibu Mkuu Hazina, aliishauri Serikali kupata kinga kutoka IPTL dhidi ya madai yanayoweza kujitokeza baada ya fedha katika akaunti ya Escrow kulipwa (**Kielelezo 22**).

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini alimwandikia Bw. Habinder Singh Sethi Mwenyekiti na Mtendaji wa IPTL barua yenye Kumb. Na.SBD.88/147/01/4 ya tarehe 20 Septemba 2013 kumtaka kuthibitisha umiliki wake wa asilimia 70 na kutoa kinga kwa Serikali, Benki Kuu na kwa TANESCO (**Rejea Kielelezo 16**).

Kupitia kikao cha tarehe 8 Oktoba 2013 TANESCO na IPTL walikaa na walikubaliana kuhusu madai ya IPTL kama ilivyonyukuliwa hapa chini “*Monies in the Escrow Account be released to IPTL as soon as possible to enable IPTL sort out its legitimate creditors as per the order of the High Court (Hon. Utamwa J.) dated 5<sup>th</sup> September, 2013. All other outstanding amounts payable to IPTL be paid in accordance with the timelines proposed herein above to enable IPTL restructure its other obligations.*”(**Kielelezo53**).

Mnamo tarehe 27 Oktoba 2013, IPTL ilitoa hati ya kinga dhidi ya madai yoyote yanayoweza kujitokeza kwa Serikali na Benki Kuu kuhusiana na fedha zilizokuwa katika akaunti ya Escrow mara baada ya fedha hizo kulipwa kwa PAP. Hati hiyo ilisainiwa na Bw. Harbinder Singh Sethi Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu na kushuhudiwa na Bw. Joseph Makandege Katibu na Wakili Mkuu wa Kampuni ya PTL.

### **2.2.3 Utolewaji wa Fedha kutoka Akaunti ya Escrow ya Tegeta**

Kwa mujibu wa makubaliano ya kuhamisha fedha za Escrow yaliyoingiwa baina ya IPTL na Wizara ya Nishati na Madini tarehe 21 Oktoba, 2013(**Rejea Kielelezo 21**), ilikubalika kuwa malipo yafanyike kuitia akaunti iliyoanishwa katika makubaliano hayo kama ifuatavyo:

**Mlipwaji:** Independent Power Tanzania Limited (IPTL)  
C/o Pan Africa Power Solutions (T) Limited  
**Benki:** UBL Bank (Tanzania) Ltd  
**Nambari ya Akaunti:** TZS-010-0016-6  
**Nambari ya Akaunti:** USD-060-0016-1

Tarehe 25 Novemba, 2013 Gavana wa Benki Kuu Prof. Beno Ndulu kupitia barua Kumb Na. NC.53/135/068/II/14 kwenda kwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPTL Bw. Harbinder Singh Sethi aliomba taarifa za kibenki za IPTL ili kufanya malipo ya fedha za Escrow (**Kielelezo 23**). Kupitia mahojiano, Gavana Prof. Benno Ndulu alibainisha kuwa Benki ilihitaji maelekezo ya mlipwaji ili kufanya malipo husika.

Kwa mujibu barua ya tarehe 25 Novemba, 2013 Kumb Na. IPTL/BOT/001/2013 Mwenyekiti Mtendaji wa IPTL Bw. Harbinder Singh Sethi alimuandikia Gavana wa Benki Kuu akiomba kuilipa IPTL fedha kutoka akaunti ya Escrow kupitia akaunti zilizoainishwa katika Makubaliano ya kuhamisha fedha baina ya Wizara na IPTL ya tarehe 21 Oktoba, 2013 ambayo yaliwasilishwa kwake. Pia alithibitisha kushiriki kikao cha tarehe 26 Novemba 2013 kilichoitishwa na Gavana (**Kielelezo 24**).

Barua kutoka Benki ya Stanbic ya tarehe 28 Novemba 2013 kwenda kwa Bw. Harbinder Singh Sethi ilimjulisha juu ya ukamilishwaji wa ufunguzi wa akaunti za PAP zifuatazo:

Jina la akaunti	Pan Africa Power Solutions (T) Ltd
Namba ya kaunti ya TZS	9120000125294
Namba ya kaunti ya USD	9120000125324
Tawi	Centre Branch
Swift Code	SBICTZTX

**(Kielelezo 25).**

Baada ya kupokea taarifa ya Stanbic tarehe 28 Novemba, 2013, Bw. Harbinder Singh Sethi alimjulisha Gavana Prof. Beno Ndulu kuwa afanye malipo husika kupitia akaunti za PAP (**Kielelezo 26**) zilizofunguliwa tarehe 28 Novemba 2013 (**Rejea Kielelezo 25**).

Baada ya Bw. Harbinder Sethi kuiandikia BoT kufanya malipo katika akaunti za PAP badala ya zile za IPTL, Mkurugenzi wa Fedha wa Benki Kuu Bw. J.R Angelo kupitia dokezo sabili katika ukurasa (folio) 12 aliomba muongozo kutoka kwa Naibu Gavana - FSD Bw. L.H Mkila na Mwanasheria wa Benki juu ya athari za kisheria endapo Benki Kuu ingelipa fedha husika katika akaunti zilizobadilishwa. Mwanasheria Bw.

Mustafa Ismail alitoa muongozo juu ya agizo la Mahakama la tarehe 5 Septemba 2013 linaloolekeza kuwa ‘all affairs of IPTL should be handed over to PAP’ pamoja na stahili za IPTL katika akaunti ya Escrow. Pia alibainisha kuwa maelekezo ya malipo (payment instructions) husika yametolewa na IPTL hivyo ni vyema Benki Kuu ikafuata maelekezo ya mwisho ya IPTL (**Kielelezo 27**).

Kikao kati ya Benki Kuu na IPTL cha tarehe 26 Novemba, 2013 kilijadili ulipwaji wa fedha kutoka akaunti ya Escrow. Ambapo kupitia Agenda Na.3.0 (ii) ilikubalika kuwa IPTL iwasilishe barua ya maelekezo juu ya ulipwaji wa fedha kutoka akaunti ya Escrow (**Kielelezo 28**).

Baada ya BoT kupokea maelekezo ya Bw. Harbinder Singh Sethi, malipo ya kwanza ya kiasi cha Sh. 8,020,522,330 na US\$ 22,198,544 yalifanyika tarehe 28 Novemba 2013 katika akaunti za PAP zilizofunguliwa katika Benki ya Stanbic (**Kielelezo 29**).

Baada ya malipo hayo kufanyika, umiliki wa hati fungani zenyenye thamani ya Sh.157,622,910,000 ikijumuisha mtaji (principal amount) wa Sh.146,567,363,967 na riba ya Sh.11,055,546,033 ulihamishwa kwenda PAP tarehe 6 Desemba, 2013 (**Kielelezo 30**). Hali kadhalika kiasi cha Shs.1,608,460,000 kutokana na kuiva kwa hati fungani Na. 158486 kilipokelewa na Benki Kuu tarehe 28/11/2013, ambapo jumla ya Sh.1,597,985,700 (1,447,614,000 + 150,371,708.48) kililipwa katika akaunti Na. 9120000125294 ya PAP iliyopo Stanbic. Tofauti ya kiasi cha Sh.10,474,300 kililipwa TRA kama Kodi ya zuio (withholding tax) kutokana na riba (**Kielelezo 90**).

Katika fedha zilizolipwa kwa PAP, kiasi cha Sh.73,573,500,000 na US\$.22,000,000 kilipwa katika akaunti Na. 00110602368802 na Na. 00151002368801 za VIP Engineering & Marketing zilizopo ‘Mkombozi Commercial Bank’ tarehe 23 Januari 2014kwa ajili ya ununuzi wa hisa asilimia 30 za VIP katika IPTL(**Kielelezo 31**).

Ilifahamika kuwa baada ya ulipwaji wa fedha zote, tarehe 28 Novemba 2013 na kuhamishwa kwa hati fungani tarehe 5 Desemba 2013, Naibu Gavana Utawala na Udhibiti wa Ndani wa Benki Kuu Bw. Juma Reli kupitia barua yenye Kumb. Na. 5746 ya tarehe 19 Desemba 2013 aliomba idhini ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Dr. Servacius Likwelile ya kufungwa kwa akaunti hiyo(**Kielelezo 32**).Nakala ya barua hiyo ilitolewa kwa Mtendaji Mkuu TANESCO, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini, Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu IPTL Bw. Harbinder Sethi na VIP Engineering & Marketing.

Baada ya kupitia Makubaliano ya akaunti ya Escrow ilibainika kuwa hakukuwa na kipengele bayana kilichoainisha kuhusu gharama za

uwakala zitakavyolipwa. Wakala hakupewa malipo yoyote kutokana na uwakala huo licha ya kuingia gharama za uendeshaji wa akaunti hizo na gharama za kisheria baada ya kushitakiwa na Bi. Martha Kaveni Renju akiiwakilisha SCB HK katika Mahakama Kuu ya Tanzania kupitia Mashauri Na.98 na Na.123 ya 2013(**Kielelezo 33**).

Kwa ujumla, BoT kama wakala iliwasiliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu Nishati na Madini na Katibu Mkuu Wizara ya Fedhawakati wa utolewaji wa fedha katika akaunti ya Escrow ili kuhakikisha kuwa ulipaji wa fedha kutoka akaunti ya ‘Escrow’ unafanyika kwa mujibu wa mkataba wa uendeshaji wa akaunti ya Escrow. Kabla ya ulipwaji wa fedha, Serikali na BoT walipewa kinga na IPTL dhidi ya madai yanayoweza kujitokeza.

#### **Mapendekezo**

- i. Benki Kuu ifanye uchambuzi wa gharama ilizoingia katika kutekeleza wajibu wake kama wakala wa uendeshaji wa akaunti ya escrowna gharama za kisheria ili iweze kufidiwa gharama hizo.
- ii. Kwa vile miamala hiyo imekwenda katika akaunti binafsi, uhakiki wa miamala ya malipo kutokea Benki Kuu na akaunti za PAP ufanywe na vyombo vyao uchunguzi ili kubaini uhalali na usahihi wake.

## **2.3 HADIDU ZA REJEA NA.3 na Na. 9**

- Kuchunguza Sababu za Kufungua Akaunti Maalumu (Escrow Account) Pia Chanzo cha Mgogoro Kuhusu Tozo Kati ya TANESCO na IPTL na Kuthibitisha Iwapo Mgogoro Uliamuliwa kwa Maslahi ya Pande zote (TANESCO na IPTL). Hii Itahusisha Kuchunguza na Kubaini Wahusika katika Mapungufu Yatakayokuwa Yamebainika Kuhusu Suala la IPTL, na
- Kuchunguza iwapo Wizara ya Nishati na Madini ambayo iliingia mkataba na IPTL wa kufungua akaunti maalum ya escrow ilifanya uadilifu na kuweka uangalifu wa kutosha kabla ya kuingia makubaliano na IPTL ya kutoa fedha zilizokuwepo kwenye akaunti hiyo na kuilipa IPTL

### **2.3.1 Sababu za Kufunguliwa kwa Akaunti ya Escrow**

Kipengele Na.6.8 (b) cha Mkataba wa kununua umeme (PPA) kinaeleza kuwa iwapo upande wowote kati ya TANESCO na IPTL utapinga usahihi wa tozo, washirika hao watalazimika kutumia jitihada zao kuhakikisha kuwa mgogoro juu ya malipo husika unamalizika kwa mujibu wa Kipengele Na 18.1 cha PPA(**Rejea Kielelezo 2**). Iwapo mgogoro huo utashindikana kutatuliwa, TANESCO itawajibika kuweka fedha yenye mgogoro kwenye akaunti ya ‘Escrow’ itakayotumika kuhifadhi fedha hizo mpaka pale mgogoro husika utakapomalizika. Pia Kipengele Na 18.2 kinaeleza kuhusu utumiaji wa mtaalamu wa upatanishi (Mediation by expert) katika utatuzi wa mgogoro kabla ya kutolewa kwa fedha zilizopo kwenye akaunti ya Escrow.

### **2.3.2. Chanzo cha Mgogoro**

Ukaguzi umebaini kuwa katika kikao cha Bodi ya Wakurugenzi wa TANESCO cha tarehe 01 Aprili 2004, TANESCO walifahamishwa na mmoja wa wanahisa wa IPTL, kampuni ya VIP kuhusu mambo kadhaa ambayo yanaashiria kuwa TANESCO inalipa viwango vya ‘tariffs’ vya juu isivyostahili. Baada ya kupata taarifa hiyo, Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO ilianza kuchunguza usahihi wake kwa kuiteua kampuni ya Mkono & Co. Advocates ili kufuutilia taarifa hiyo na kutoa ushauri. Pia Bodi iliwaateua (mionganini mwa wajumbe wa Bodi) Bw. Anorld Kilewo, Dr. Enos Bukuku na Bw.B. Mrindoko kuunda kamati maalumu ili kufuutilia kwa ukaribu taarifa hizo(**Kielelezo 34**).

Baada ya kugundua kuwa wanatozwa ‘capacity charges’ kubwa, Menejimenti ya TANESCO tarehe 17 Juni 2004 ilitoa tamko la kugomea ankara za IPTL kwa barua Na.DMDF&CS/02/05 (**Rejea Kielelezo 4**) baada ya kupokea ushauri kutoka kwa Mkono & Co. Advocates (**Kielelezo 35**) na kisha kufungua akaunti ya Escrow kulingana na kipengele Na. 6.8(b) cha PPA.

Tarehe 17 June, 2004 aliyejekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO wa wakati huo Bw.C.G.N Huysen alimtaarifu aliyejekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO Bw. Ndewirwa N. Kitomari kuitia barua yenye Kumb.Na.SEC.427/06/2004 juu ya uamuji wa kikao maalum cha Bodi ya Wakurugenzi kilichokaa tarehe 01 Aprili, 2004 wa kuiteua kampuni ya M/s Mkono & Co. Advocates kuchunguza na kutoa maoni ya kisheria kuhusu gharama za uwekezaji zinazotozwa na IPTL. Pia katika barua hiyo alimtaarifu Mwenyekiti wa Bodi kuwa TANESCO imeanza kugomea gharama za uwekezaji za IPTL zenyenye mgogoro kwa kutoa 'Invoice Dispute Notices' (Kielelezo 36).

Katika kikao chake cha tarehe 30 Juni, 2004 Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO ilialika kampuni ya Mkono & Co. Advocates kuwasilisha taarifa ya uchunguzi kuhusu gharama za uwekezaji zinazotozwa na IPTL (Kielelezo 37).

### **2.3.3 Ushauri wa Mkono &Co. Advocates kuhusu gharama za uwekezaji**

Baada ya Kampuni ya Mkono & Co. Advocates kukamilisha uchunguzi, tarehe 30 Juni, 2004 ilitoa maoni ya kisheria kwa Bodi ya TANESCO kuhusu gharama za uwekezaji zinazolipwa na TANESCO (*Legal Opinion on Tariff payable by TANESCO to IPTL under Power Purchase Agreement*) (Rejea Kielelezo35).

Katika maoni hayo,TANESCO ilishauriwa kutokubaliana na ankara za malipo ya gharama za uwekezaji zitakazowasilishwa na IPTL baadaya kubainika kwamba kiwango cha tozo hizo hukokotolewa kwa kuzingatia mtaji wa wanahisa (Owners Equity) Dola za Kimarekani Milioni 38.16 badala ya Shilingi za Kitanzania 50,000 pekee kiasi ambacho pia kilisajiliwa na Msajili wa Makampuni (BRELA). Pia kiasi hicho kimeoneshwakatika hesabu (Financial Statements) za IPTL zilizokaguliwa kwa mwaka 2002 hadi mwaka2007(Kielelezo 38 na Rejea Kielelezo 5).

Mapendekezo ya Mkono & Co. Advocates katika kipengele cha 7 na 8 katika taarifa yake kwa Bodi aliishauri TANESCO kuwataka IPTL kufanya marekebisho ya gharama za uwekezaji (Capacity Charges) kwa kuzingatia mtaji wa Shilingi 50,000 na kuanzisha madai dhidi ya IPTL ili kurejesha fedha zilizolipwa zaidi kutokana na kutumika kwa mtaji wa Dola za Kimarekani Milioni 38.16 katika ukokotoaji wa tozo za uwekezaji isivyosahihi. Pia TANESCO ilishauriwa kutoa tamko la kutokubaliana na tozo hiyo (Invoice Dispute Notice) na endapo hakutakuwa na suluhisho, TANESCO na IPTL wangepaswa kufungua akaunti maalumu ya Escrow kwa haraka kwa mujibu wa Kipengele Na. 6.8 (b) cha PPA(Rejea Kielelezo 35 na Kielelezo 5 na Kielelezo 2).

### **2.3.4 Uchunguzi na Ushauri wa Kamati Ndogo ya Bodi ya TANESCO Kuhusu**

### **Mgogoro wa Gharama za Uwekezaji**

Baada ya kupokea taarifa toka kwa VIP kuhusu malipo ya ‘capacity charges’ yanayofanyika, Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO katika kikao chake cha tarehe 01 Aprili, 2004 iliunda kamati ndogo maalumu ya kuchunguza madai juu ya TANESCO kutozwa zaidigharama za uwekezaji. Kamati hiyo iliyoundwa na Bw. Arnold.B.S Kilewo, Bw. B. Mrindoko na Dk. Enos S. Bukuili iliandaa taarifa na kuiwasilisha katika kikao cha Bodi Na.446 kilichokaa tarehe 13 Agosti 2004 (**Rejea Kielelezo 38**).

Taarifa ya Kamati iliainisha kuwa wanahisa wa IPTL hawakuwekeza kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 38.16 ambacho pia kilitumika kukokotolea gharama za uwekezaji, badala yakewaliwekeza Shilingi 50,000 kama mtaji wa wanahisa(**Rejea Kielelezo 5**).

Kamati ilibainisha kuwa kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 38.16 kilikuwa ni mkopo wa wanahisa kwa kampuni na kilikuwa kinarejeshwa kama mkopo na sio kama gawio (dividends). Hivyo kamati iliishauri Wizara ya Nishati na Madini kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuitisha mazungumzo baina ya pande zote mbili ili kutatua mgogoro huo (**Kielelezo 39**).

Baada ya kupata ushauri kutoka Mkono & Co. Advocates na Kamati Maalum, Bodi ya TANESCO katika kikao chake cha tarehe 13 Agosti 2004 iliazimia kupata maoni mengine ya kisheria kutoka kwa Hunton & Williams ambao ni mawakili wa TANESCO katika shauri la ICSID.

#### **2.3.5 Ushauri wa Kisheria kutoka kwa Hunton and Williams LLP Kuhusu Mgogoro walIPTL na TANESCO**

Katika uchunguzi wao Hunton and Williams waliainisha kuwa ujenzi wa mitambo ya IPTL kwa kutumia mtaji (Owners Equity) wa TShs 50,000 haileti mantiki katika uhalisia wake kinyume na ilivyoinishwa na Mkono & Co. Advocates. Vilevile Hunton and Williamslibainisha kuwa mtaji wa USD 38.16 Milioni uliokuwa ukitumiwa na IPTL katika ukokotoaji wa ‘capacity charges’ haukuthibitika usahihi wake kama ilivyokuwa imeamuliwa katika Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi ICSID tarehe 12 Julai 2001 (ICSID 1). Hata hivyo kwa kutolipa gharama za uwekezaji (capacity charges), TANESCO hawakuwa na nafasi ya kushinda katika shauri hilo na hivyo kushauriwa kukaa pamoja na IPTL kujadili na kukubaliana juu ya mtaji halisi uliowekezwa na wanahisa (Owners equity)(**Kielelezo 40**).

Kupitia barua yenye Kumb Na. SEC.427/09/2004 ya tarehe 23 Septemba, 2004 aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO Bw. C. G .N Huysen alimjulisha Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini kuhusu ushauri wa kisheria uliopokelewa na TANESCO kutoka kwa Mkono &Co.Advocates na

Hunton and Williams. Kwa kuwa ushauri uliotolewa na Mkono & Co. Advocates ultifautiana na ule uliotolewa na Hunton and Williams, TANESCO iliiomba Wizara kusaidia kuomba ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali (**Kielelezo 41**).

#### **2.3.6 Hatua Zilizochukuliwa na Menejimenti ya TANESCO kabla ya Kufunguliwa kwa Akaunti ya Escrow**

Kufuatia maoni ya kisheria ya Mkono & Co. Advocates kutofautiana na maoni ya Hunton and William LLP, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Bw.C.G.N Huysen alimuomba ushauri Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia barua Na. SEC.247/07/04 ya tarehe 05 Julai 2004 ambapo ushauri wa Mkono & Co. na Hunton and William uliambatanishwa (**Kielelezo 42**).

Kufuatia kutojibowi kwa barua Na. SEC.247/07/04 ya tarehe 05 Julai 2004 na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Bw.C.G.N Huysen alimuomba Katibu Mkuu Nishati na Madini kupitia barua Na. SEC.427/9/2004 ya tarehe 23 Septemba 2004 (**Rejea Kielelezo 41**) kuwasiliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupata majibu ya Barua Na. SEC.247/07/04 ya tarehe 5 Julai 2004 (**Rejea Kielelezo 42**).

Pia Mkurugenzi Mtendaji alimuomba ushauri Msajili wa Hazina kupitia barua Na. SEC.427/8/2004 ya tarehe 16 Agosti 2004 kufuatia mgongano huo wa maoni ya kisheria (**Kielelezo 43**).

Barua Na. NEM/740/05 ya tarehe 06 Desemba 2005 kutoka kwa Mkono & Co. Advocates kwenda kwa Katibu Mkuu wa Nishati na Madini Bw. Patrick Rutabanzibwa ilirejea mazungumzo ya tarehe 05 Desemba 2005 ambapo iliamuliwa kuwa Kampuni ya Mkono & CO. Advocates iandae rasimu ya makubaliano kwa ajili ya ufunguzi wa akaunti ya Escrow (**Kielelezo 44**).

Makubaliano ya kufungua akaunti ya Escrow yaliingiwa tarehe 5 Julai 2006na akaunti hiyo kufunguliwa katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa mujibu wa Kipengele Na.6.8(b) cha PPA. Ambapo Kampuni ya IPTL na Wizara ya Nishati na Madini ndiyo waliokuwa washirika na BoT ikiwa wakala katika makubaliano husika.

#### **2.3.7 Madai ya kampuni ya PAP ya kutaka kulipwa fedha kutoka akaunti ya Escrow**

Baada ya hukumu ya Mahakama Kuu ya Tanzania katika Shauri Na.49 la 2002 na Na.254 la 2003 ya tarehe 5 Septemba, 2013 Mkurugenzi Mtendaji wa PAP, Bw. Harbinder Singh Sethialimuandikia Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO barua Na.IPTL/GEN/002-2013 ya tarehe 13 Septemba, 2013

kumtaka kulipa pesa zote zilizokuwa kwenye akaunti ya Escrow kufuatia hukumu hiyo(**Kielelezo 45**).

Aidha barua yenyne Kumb. Na.IPTL/TANESCO/2013/03 ya tarehe 18 Septemba, 2013 ilioandikwa na Bw. Harbinder Sethi kwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO ilisisitiza kutolewa kwa fedha za Escrow na TANESCO kutoendelea kupinga ankara za Madai (**Kielelezo 46**).

### **2.3.8 Hatua na Tahadhari zilizochukuliwa na Wizara kabla ya utoaji wa Fedha katika akaunti ya Escrow**

#### **(i) Kuomba Ushauri kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kabla ya kutekeleza maombi ya IPTL, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini Bw.EliakimC. Maswi kupitia barua yenyne Kumb Na. CBD.88/147/29 ya tarehe 16 Septemba, 2013 alimwandikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuomba ushauri katika masuala yafuatayo (**Kielelezo 47**):

- a) Kwamba haamini kama fedha zote zilizomo katika akaunti ya Escrow ni za PAP kwa vile fedha hizo ziliwekwa katika akaunti hiyo kutokana na mgogoro wa tozo za ‘capacity charges’ kati ya TANESCO na IPTL, na hivyo umiliki wa fedha hizo utafahamika pale tu mgogoro huo utakapokuwa umetatuliwa.
- b) Kwamba PAP atastahili kupata kiasi kinachotakiwa kulipwa kwa IPTL baada ya mgogoro huo kutatuliwa na sio kiasi chote kilichokuwepo katika akaunti ya escrow kama inavyodaiwa na PAP. Hivyo, akashauri kuwa pande mbili katika mkataba wa escrow zikae na kujadili suala husika ili kupata ufumbuzi wake.

#### **(ii) Kuitaka PAP kuthibitisha umiliki wa Hisa za Mechmar katika IPTL na Kutoa kinga kwa Serikali dhidi ya madai yatokanayo na utolewaji wa fedha katika akaunti ya Escrow**

Tarehe 20 Septemba 2013 Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini alimjulisha Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa IPTL Bw. Harbinder Singh Sethi ambaye pia ni mmiliki wa PAP kupitia barua yenyne Kumb. Na. SBD.88/147/01/4, kuwa Wizara haikuwa na pingamizi dhidi ya kutolewa kwa fedha za Escrow kama Bw. Sethi angetekeleza yafuatayo (**RejeaKielelezo 16**);

- a) Kuwasilisha ushahidi wa kuuzwa kwa hisa asilimia 70 za Mechmar katika IPTL.

b) IPTL kutoleta madai mengine kwa Serikali au TANESCO juu ya fedha za Escrow baada ya malipo.

Bw. Harbinder Sethi aliwasilisha ‘Deed of Assignment of Shares’ na Mkataba wa Kuza na Kununua hisa kati ya PAP na PiperLink Investment kutokana na agizo la kuwasilisha ushahidi wa kununua asilimia 70 za hisa za Mechmar katika IPTL (**Kielelezo 48**).

**(iii) Kuitaka IPTLkutoa Kinga Dhidi ya Madai Yatokanayo na KulipwaFedha Kutoka Akaunti ya Escrow**

Kabla ya kutolewa kwa fedha katika akaunti ya Escrow, IPTL ilitoa kinga dhidi ya madai yanayoweza kutokea baada ya kulipwa fedha zilizokuwa katika akaunti ya Escrow (**Kielelezo 49**).

**(iv) Kuitisha Kikao cha Wadau Mbalimbali**

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini Bw. Eliakim Maswi kupitia barua yenye Kumb Na. CDB.88/417/31 ya tarehe 23 Septemba, 2013 alimwandikia Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, kumuomba kuitisha kikao kilicholenga kujadili suala la umiliki wa fedha za Escrow (**Rejea Kielelezo 18**). Kikao hicho kilihudhuriwa na maofisa kutoka Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini, Benki Kuu na TANESCO.

Katika kikao hicho, iliundwa timu ya wataalamu ili kuchambua na kutoa ushauri wa namna ambavyo fedha za Escrow zingelipwa kwenda kwa IPTL; ambapo kwa barua yenye Kumb. Na. CAC/184/211/01/23 ya tarehe 30 Septemba, 2013 timu husika ilitoa taarifa yake na kupendekeza kuwa IPTL na TANESCO wanapaswa kutatua mgogoro wa ankara za ‘capacity charges’ na mambo yanayohusiana na mgogoro huo kisha kuwasilisha makubaliano ya pamoja (**Rejea Kielelezo 19**).

### **2.3.9 Ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Katika ushauriwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mh. Jaji Frederick M. Warema alipendekeza kuwa washirika wa akaunti ya Escrow wakutane ili kutatua migogoro yao na kutumia wataalam wa masuala ya kifedha ili kubaini kiasi stahili kinachopaswa kurejeshwa TANESCO. Pia Mwanasheria Mkuu alishauri dhamana iliyotolewa na Serikali katika PPA iangaliwe upya kulingana na mazingira yaliyopo (**Rejea Kielelezo 17**).

### **Utekelezaji wa Ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Baada ya ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu hukumu ya Mahakama Kuu ya Tanzania (Mh.Jaji Utamwa) kumfikia Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Bodi ya Wakurugenzi wa TANESCO ilikaa kikao cha dharura tarehe 19 Septemba 2013 na kujadili suala la utolewaji wa fedha katika akaunti ya Escrow. Katika kikao hicho Menejimenti ya

TANESCO iliwasilisha taarifa Na. 4447 ambapo Menejimenti ilitahadharisha juu ya utolewaji wa fedha katika Akaunti ya Escrow kabla ya kuhitimishwa kwa shauri la madai ya msingi ya TANESCO juu ya ‘capacity charges’(**Kielelezo 50**).

Katika kikao hicho, Bodi ya TANESCO ilikubaliana na ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ulioitaka TANESCO na IPTL kukaa na kutatua madai yanayohusu Akaunti ya Escrow na kubainisha kiasi kinachostahili kulipwa kwa pande husika.

Baada ya kikao hicho, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO Jenerali Mstaafu Robert P. Mboma alimwandikia Katibu Mkuu wa Nishati na Madini barua Na. SEC.427/IPTL/9/2013 ya tarehe 19 Septemba 2013 akibainisha kuwa TANESCO itafuata maelekezo ya Mwanasheria Mkuu na kwamba washirika wa akaunti ya Escrow watacaa kwa pamoja kutatua mgororo wa tozo ya gharama za uwekezaji (Capacity charges) ili kubaini kiasi kinachopaswa kurejeshwa TANESCO na kile kinachostahili kulipwa IPTL. Hivyo Bodi ya Wakugenzi ya TANESCO ilitoa mchanganuo wa madai yaliyopaswa kuhakikiwa kwanza ndipo yalipwe kwa IPTL(**Kielelezo 51**).

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini kufuatia barua ya IPTL ya kudai kulipwa zaidi ya kiasi kilichokuwemo katika akaunti ya escrow, alimjulisha Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mhandisi Felchesmi Mramba kuhusu madai ya IPTL kuitia barua Na.BD.88/417/01/76 ya 9 Oktoba, 2013 na kuagiza TANESCO kufanya kikao na IPTL ili kujadili madai hayo na kuwa uamuzi utakaotokana na majadiliano hayo utasaidia utolewaji wa fedha katika akaunti ya Escrow (**Kielelezo 52**).

TANESCO na IPTL walikaa katika kikao cha tarehe 8 Oktoba 2013 na kukubaliana kuhusu madai ya IPTL ya USD 79,049,724.50(**Kielelezo 53**). Katika Kikao hicho TANESCO iliomba kuondolewa kwa kiasi cha USD 33,564,004.53 ambacho kilikuwa ni riba na adhabu itokanayo na malimbikizo ya tozo ya gharama za uwekezaji. IPTL ilikubaliana na ombi hilo endapo TRA ingeisamehe kodi ya kiwango sawa na hicho.

Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO enerali Mstaafu Robert Mboma kuitia barua Na. SEC.427/IPTL/10/2013 ya tarehe 9 Oktoba 2013 alijulisha Wizara kuwa IPTL ingeidai TANESCO kiasi cha USD.45,485,719.97 (endapo TRA itasamehe kodi kiasi cha USD 33,564,004.53) ama USD 79,049,724.50 (endapo hakutakuwa na msamaha wa kodi) zaidi ya kiasi kilichopo katika akaunti ya Escrow ya Tegeta(**Kielelezo 54**).

Baada ya kupokea mapendekezo ya Bodi ya TANESCO kuwa fedha katika akaunti ya Escrow zilipwe kwa IPTL, tarehe 21 Oktoba, 2013 Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini Bw. Eliakim Maswi pamoja na Mwanasheria wa Wizara hiyo Bi. Salome Makange kwa niaba ya Serikali waliingga

makubaliano na Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji Bw. Harbinder Singh Sethi na Mwanasheria wa IPTL Bw. Joseph Makandege juu ya utolewaji wa fedha katika akaunti ya Escrow (Agreement for delivery of funds to Independent Power Tanzania Limited (IPTL) (**Rejea Kielelezo 21**).

#### **Mapendekezo**

- Mwanasheria Mkuu wa Serikali achukue hatua stahili ili kuhakikisha kwamba Serikali na Benki Kuu ya Tanzania zinakingwa dhidi ya madai yoyote yanayoweza kujitokeza kwa kutumia kinga iliyotolewa na IPTL.
- Serikali ihakikishe inapitia upya dhamana (guarantee) iliyotolewa katika utekelezaji wa mkataba wa uzalishaji wa umeme ili kuiepusha Serikali na hasara kutohana na mambo yasiyotarajiwa

## 2.4 HADIDU ZA REJEA NA.4, 5 na 10

Kuchunguza kama Wakati wa Kufungua Akaunti Maalum ya BoT (Akaunti Escrow) Mechmar Ilikuwa Inamiliki IPTL. Pia, Kuthibitisha Kwamba Kampuni ya Mechmar Ilikuwa Imehamishia Umiliki wake kwa Kampuni ya PAN AFRICA Power Solution (T) Limited (PAP) Kabla ya Kufilisiwa na Kwamba Sasa PAP inamiliki IPTL

### 2.4.1 Kampuni ya Mechmar na Uanzishwaji wa IPTL

Kampuni ya Mechmar ilisajiliwa nchini Malaysia tarehe 19 Desemba, 1972 (ikiitiwa Mechmar Bestobell Bhd) kwa Na.13380-M ikijihuisha na utoaji wa Huduma za Menejimenti ya Makampuni. Mechmar ilikuwa na jumla ya wanahisa ishirini na moja (21) na jumla ya mtaji wa Malaysian Ringgit (RM) 149,646,000 kutoka katika hisa 1,496,460 (**Jedwali T6**).

#### **Jedwali T6: Orodha ya Wanahisa wa Mechmar Corporation na Idadi ya Hisa**

Na.	Kampuni Na.	Jina la Mmiliki	Thamani ya Hisa
1	17521-U	Mekmore SDN BHD	1,958,800
2	S0397375A	Quek Keng Seng	926,029
3	6464-T	Public Nominees (Temparatan) SDN. Bhd	1,958,800
4	284597-P	Maybank Securities Nominees (Temparatan). Bhd	1,637,899
5	591105-10-6117	Johnny Soon Choon Jeen	902,200
6	258939-H	Maybank Nominees (Temparatan) SDN Bhd	6,779,300
7	9969-D	Kam Loong Mining SDN. Berhad	10,823,000
8	600126-10-6281	Kam Chan Seng	2,415,900
9	281204-12-5029	Philip Lai	934,700
10		Shareholders for Berhad Company	50,491,810
11	258515-D	Amsec nominees (Asing) SDN. Bhd	929,000
12	270268-W	Hlib Nominees (Tempatan) Sdn. Bhd	25,275,700
13	490129-10-5263	Tan Kee Huat	1,500,000
14	550515-08-5688	Leong Wai Yien	1,300,000
15	263875-D	Citicorp Nominees (Asing) Sdn. Bhd	7,307,500
16	268290-H	Ta Nominees (Tempatan) Sdn. Bhd	800,533
17	26777-T	Mercsec Nominees (Tempatan) Sdn. Bhd	1,034,000
18	730727-08-5805	Tan Yu Wei	1,800,000
19	390321-10-5382	Lily NG @ NG HUI CHIN	2,244,000
20	102918-T	Amsec Nominees (Tempatan) Sdn. Bhd	27,621,829
21	500317-09-5011	Mohamed Fauzy Bin Abdullah	1,005,000
Jumla ya hisa zilizouzwa na kununuliwa			<b>149,646,000</b>

(Kielelezo 55).

Tarehe 15 Desemba, 1973 na 26 Septemba, 1981 Bw. Tan Kean Wan (IC/Passport Na. 430225-08-5421) na Bw. Baharuden Bin Abd Majid Datuk (IC/Passport Na.530422-04-5355) waliteuliwa kuwa wakurugenzi wa Mechmar (Rejea Kielelezo 55).

Hata hivyo Kampuni ya Mechmar iliwekwa katika ufilisi na Mahakama Kuu ya Malaya, Kuala Lumpur kuanzia tarehe 18 Mei 2012 kufuatia Shauri la Madai Na. 28NCC-223-03/2012 lilofunguliwa na Alliance Investment Bank Berhad dhidi ya Mechmar Corporation (Malaysia) Berhad, ambapo Bw. Heng Ji Keng na Bw. Joseph Monteiro wa Ferrier Hodgson MH waliteuliwa kuwa wafilisi (**Kielelezo 56**).

Kampuni ya IPTL ilianzishwa na kusajiliwa Tarehe 1 Novemba, 1994 kwa malengo ya kuzalisha na kuuza umeme (**Kielelezo 57**). Kampuni hii ilikuwa inamiliwiwa na wanahisa wawili ambao ni Mechmar Corporation Malaysia Berhad (Mechmar) na VIP Engineering and Marketing Limited (VIP). Wakati IPTL ilipoanzishwa, Mechmar ilikuwa na hisa saba (7) sawa na asilimia sabini (70) na VIP ilikuwa na hisa tatu (3) sawa na asilimia thelathini (30). Mechmar ilichangia mtaji (Shareholders Equity) wa Sh. 35,000 kwa kununua hisa saba (7) na VIP Sh. 15,000 kwa kununua hisa tatu (**Kielelezo 58**).

#### **2.4.2 Umiliki wa Mechmar kwa IPTL wakati wa kufungua Akaunti ya Escrow**

Kwa mujibu wa taarifa za marejesho ya kila mwaka (Annual Returns) za IPTL zilizowasilishwa BRELA zinaonesha kuwa hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2006 (**Kielelezo 59**) mwaka ambao Akaunti ya Escrow ilifunguliwa, wamiliki wa IPTL walikuwa ni Mechmar na VIP.

Kwa kipindi hicho Mechmar iliwakilishwa na Bw. Datuk Baharuden Majid katika Menejimenti ya IPTL ambaye ndiye aliyeweka sahihi katika makubaliano ya kufungua akaunti ya Escrow. Hivyo kwa kuzingatia ushahidi uliopatikana katika nyaraka husika, Mechmar ilikuwa mmiliki halali wa IPTL wakati akaunti ya Escrow ilipofunguliwa (**Rejea Kielelezo 6**).

Pamoja na kuwa wakati wa kuingwa kwa makubaliano ya akaunti ya Escrow tarehe 5 Julai 2006 kampuni ya IPTL ilikuwa katika mgogoro wa wanahisa kati ya VIP na Mechmar ulioanza mwaka 2002 na kupelekea kufunguliwa kwa shauri la ufilisi, Kampuni ya Mechmar ilikuwa mwanahisa wa IPTL kwa asilimia 70 hadi kufikia 2013.

#### **2.4.3 Mauzo ya Hisa saba (7) za Mechmar na tatu (3) za VIP katika IPTL**

##### **i. Uuzaji wa Hisa za Mechmar katika IPTL kwenda Piper Link**

Kwa mujibu wa Mkataba uliowasilishwa na Bw. Harbinder Sigh Sethi katika taasisi mbalimbali za Serikali uliosainiwa tarehe 9 Septemba 2010, Mechmar iliingia Makubaliano na Piper Link Investment ya British Virgin Islands (BVI) juu ya uuzwaji wa hisa saba (7) za IPTL kwa gharama ya US\$. 6,000,000 (**Kielelezo 60**).

Makubaliano hayo yaliwekwa saini mbili kwa niaba ya Mechmar na saini moja kwa niaba ya Piper Link Investment. Watia saini katika Makubaliano husika hawakuainisha majina yao dhidi ya sahihi zilizowekwa (**Rejea Kielelezo 60**).

**ii. Uuzwaji wa Hisa za Mechmar katika IPTL kutoka kwa Piper Link Investment kwenda kwa Pan Africa Power Solution (T) Ltd (PAP)**

Baada ya Kampuni ya Piper Link Investment kununua hisa saba (7) za Mechmar katika IPTL tarehe 9 Septemba 2010 kwa US\$.6,000,000 (**Rejea Kielelezo 60**), kampuni ya PAP iliingia makubaliano ya kuhamishiwa umiliki wa hisa saba (7) za IPTL kutoka Piper Link Investment tarehe 21 Oktoba 2011 kwa gharama ya US\$.20,000,000. Hati ya kuhamishiwa hisa husika (Deed of Assignment of Shares) inaonyesha kusainiwa na Issa Al Rawahy Mkurugenzi na kushuhudiwa na Bw. Santosh Shetty Meneja Mauzo, Bw. Raj Shetty Mtendaji Mkuu Mauzo kwa niaba ya Piper Link Investment, na kusainiwa na Bw. Harbinder Singh Sethi Mkurugenzi Mkuu, Manraj Singh Bharya Mkurugenzi kwa niaba ya PAP na kushuhudiwa na Wakili Augustine Kusalika (**Rejea Kielelezo 60**).

Katika kipindi cha mauzo hayo kampuni ya Mechmar haikuwa katika ufilisi kwani Mechmar iliwekwa katika ufilisi nchini Malaysia mwaka 2012.

Martha Renju ambaye tarehe 15 Desemba 2008 na 23 Januari 2009 aliteuliwa na SCBHK kuwa Msimamizi wa Hisa (Official Share Receiver) za VIP na baadae za Mechmar katika IPTL alifungua Shauri Na. BVIH COM 2010/147 katika Mahakama Kuu ya British Virgin Islands (BVI) tarehe 8 Novemba 2010 ambapo siku hiyo hiyo amri ya Mahakama (Jaji Edward Bennister) ya kusitishwa uuzaaji wa hisa saba (7) za Mechmar katika IPTL kwenda Piper Link Investments ilitolewa (**Kielelezo 61**).

Kutokana na uamuvi huo wa mahakama kuzuia mauzo ya hisa za Mechmar, hati ya hisa hizo iliwasilishwa mahakamanitarehe 30 Novemba 2010 (**Kielelezo 62**) natarehe 13 Aprili 2011 baada ya uamuvi wa mwisho wa mahakama, hati ya hisa saba za Mechmar ilikabidhiwa kwa Martha Renju kupitia wanasheria Maples and Calder (**Kielelezo 63 na 64**).

Ilibainika kupitia hati ya kuhamisha hisa (deed of assignment of shares), PiperLink Investment iliingia makubaliano na PAP ya kuuza hisa hizo wakati hisa hizo zikiwa zimezuiwa kutokana na maamuvi ya mahakama ya BVI. Vilevile Kampuni ya PAP iliingia makubaliano hayo wakati ambapo mahakama ya BVI ikiwa imezuia uuzwaji wa hisa

husika. Wakati wa makubalino hayo yanafanyika kampuni ya IPTL ilikuwa katika ufilisi.

Kufuatia mgogoro mionganoni mwa wanahisa wa IPTL, VIP ilifungua Shauri la Madai Na.49 la 2002 ikiomba kufilisiwa kwa IPTL kwa amri ya Mahakama. Tarehe 5 Septemba, 2013 iliamuliwa na Mahakama Kuu ya Tanzania chini ya Mh. Jaji Utamwa (Shauri Na. 49 la 2002 na Na.254 la 2003) kwamba Kampuni ya IPTL ikabidhiwe kwa PAP baada ya VIP kuondoa ombi la ufilisi Mahakamani (**Rejea Kielelezo 7**).

Kwa mujibu wa hukumu hiyo, Kampuni ya PAP ilimilikishwa kampuni ya IPTL na masuala yote yahusuyo IPTL.

### **iii. Mauzo ya Hisa za VIP katika IPTL kwenda PAP**

Tarehe 15 Agosti 2013 kampuni ya VIP iliingia makubaliano na PAP ya kuuza hisa tatu (3) katika IPTL, ambapo utekelezaji wa makubaliano hayo ulianza rasmi tarehe 19 Agosti 2013 kulingana na Kipengele Na. 1.26 cha Makubaliano ya Uuzaji na Ununuzi wa Hisa hizo (**Kielelezo 65**). Wakati wa makubalino hayo yanafanyika kampuni ya IPTL ilikuwa katika ufilisi. Mahakama Kuu ya Tanzania iliridhia (taking judicial notice) makubaliano hayo katika hukumu ya tarehe 5 Septemba 2013.

#### **2.4.4 Kodi ya Ongezeko la Mtaji (Capital Gain)**

Kodi ya ongezeko la mtaji ni kodi ambayo hutozwa kwenye faida inayotokana na mauzo ya mali (property) na uwekezaji (investment) na katika faida ipatikanayo kwa mauzo ya hisa. Kodi ya Ongezeko la mtaji inalipwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 90 cha Sheria ya Kodi ya Mwaka 2006 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2012).

#### **Kodi ya Ongezeko la Mtaji kutokana na Uuzwaji wa Hisa za Mechmar Kwenda Piper Link Investment**

Kwa mujibu wa “share sale agreement” kampuni ya Mechmar Corporation iliuza hisa zake 7 ilizokuwa inamiliiki katika kampuni ya IPTL kwa kampuni ya Piper Link Investment kwa kiasi cha Dola za kimarekani 6,000,000 tarehe 9 Septemba, 2010 (**Kielelezo 66**).

Hata hivyo taarifa zilizowasilishwa TRA na PAP zilionyesha kuuzwa kwa hisa hizo kwa kiasi cha shilingi za Kitanzania 6,000,000 tofauti na kiasi kilichoainishwa katika mkataba cha USD 6,000,000 (**Kielelezo 67 na Rejea Kielelezo 66**).

Baada ya kupokea taarifa za Mechmar zilizowasilishwa na PAP, TRA ilikokotoa kodi husika ambapo kupitia barua Kumb. Na. TRA/DR/ILA/RE/175ya tarehe 15 Novemba, 2013 kwenda kwa Mechmar iliyosainiwa kwa niaba ya Meneja wa TRA Mkoa wa Kikodi wa Ilala na Bw.

Paschal Kabundunguru, TRA waliiarifu Mechmar kuwa inapaswa kulipa kodi ya “capital gain” kiasi cha Sh.596,000 kutokana na mauzo ya hisa zake kwa kampuni ya Piper Links Investments Ltd. Kiasi hicho cha kodi kilikokotolewa kwa kuzingatia mauzo ya kiasi cha Shilingi 6,000,000. Pia TRA iliiarifu Mechmar kuwa kiasi cha ziada cha Shilingi 180,000 kilipaswa kulipwa kama adhabu na stamp duty, hivyo jumla ya kiasi cha Shilingi 776,000 kilitozwa na kukusanywa kuititia benki ya CRDB akaunti Na. 01J1042989549 tawi la WaterFront tarehe 6 Desemba, 2013 (**Kielelezo 68 na Rejea Kielelezo 67**).

Taarifa hizo zilionyesha kwamba hisa hizo ziliuzwa kwa Piper Link tarehe 9 Septemba, 2013 badala ya tarehe 9 Septemba, 2010 iliyoinishwa kwenye “Share Sale Agreement” (**Rejea Kielelezo 66 na 67**).

**Kodi ya Ongezeko la Mtaji kutokana na Uuzwaji wa Hisa Kutoka Kampuni ya Piper Link Investment Kwenda PAP**

Kwa mujibu wa “deed of assignment of shares” ya tarehe 21 Oktoba, 2011 iliyowasilishwa na Bw. Harbinder Singh Sethi katika taasisi mbalimbali za serikali, Kampuni ya Piper Link Investment iliuzia Kampuni ya PAP hisa 7 katika IPTL kwa Dola za Kimarekani 20,000,000 (**Rejea Kielelezo 60**).

Hata hivyo kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa TRA, hisa 7 za IPTL ziliuzwa na Piper Link Investment kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 300,000 (**Rejea Kielelezo 67**).

Tarehe 15 Novemba 2013 kuititia barua Kumb. Na. TRA/DR/ILA/RE/175, TRA iliiarifu Piper link kuwa inapaswa kulipa kodi ya ongezeko la mtaji ya kiasi cha Shilingi 47,940,000 kutokana na mauzo ya hisa 7 katika IPTL kwa kampuni ya PAP kwa bei ya Dola za Kimarekani 300,000. Pia TRA iliiarifu Mechmar kuwa kiasi cha ziada cha Shilingi 4,800,000 kilipaswa kulipwa kama ‘stamp duty’. Hapakuwa na tozo kwa adhabu ya kuchelewa. Kwa barua hiyo ya TRA, inaonesha hisa hizo ziliuzwa kutoka kwa Piper Link kwenda kwa PAP tarehe 30 Oktoba, 2013 badala ya tarehe 21 Oktoba, 2011 kama ilivyoainishwa katika “deed of assignment of shares” (**Kielelezo 69**).

Tarehe 6 Desemba, 2013 jumla ya kiasi cha Shilingi 62,340,000 (47,940,000 + 14,400,000) kama kodi hiyo kililipwa TRA kuititia Akaunti Na. 01J1042989549 benki ya CRDB tawi la WaterFront (**Kielelezo 70**).

TRA ilibainisha kuititia memoranda yenyeye kumb Na. 03-2013-2014-975 ya tarehe 18 Juni, 2014 kuwa jumla ya kiasi cha Sh. 53,445,300 cha kodi ya Ongezeko la Thamani na ‘Stamp Duty’ kililipwa badala ya Sh. 8,735,966,400. Ambapo jumla ya kiasi cha Sh. 8,682,521,100 (**Jedwali**

**T7) hakikulipwa na Kampuni za Mechmar Corporation na Piper Link Investment (Kielelezo 71).**

Mnamo tarehe 16 Septemba 2014 kiasi cha Sh. 411,140,000 kililipwa na PAP kupitia Benki of India (T) Limited kwa ajili ya ushuru wa stempu (Kielelezo 72).

**Jedwali T7: Mchanganuo wa Kodi ya Ongezeko la Mtaji na Ushuru wa Stempu**

Maelezo	Ongezeko la Mtaji		Ushuru wa Stempu		Jumla		Grand Total
	Mechmar (Sh.)	PLI (Sh.)	Mechmar (Sh.)	PLI (Sh.)	Mechmar	PIL	
Kilicholipwa	596,500	47,988,800	60,000	4,800,000	656,500	52,788,800	53,445,300
Kinachopaswa kilipwa	1,919,988,800	6,399,977,600	96,000,000	320,000,000	2,015,988,800	6,719,977,600	8,735,966,400
Kinachodaiwa	1,919,392,300	6,351,988,800	95,940,000	315,200,000	2,015,332,300	6,667,188,800	8,682,521,100

Pia ripoti hiyo ilibainisha kuwa Kodi ya Ongezeko la Mtaji ililipwa kwa kiwango cha asilimia 10 kama kampuni iliyosajiliwa nchini Tanzania badala ya asilimia 20 inayopaswa kulipwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 90 cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332 (R.E 2006) kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha Na.8 ya Mwaka 2012 kwa kampuni zilizosajiliwa nje ya nchi.

Pia TRA walibaini kuwa msingi wa ukokotoaji wa kiwango cha kulipa Kodi ya Ongezeko la Mtaji ultokana na nyaraka zenye taarifa zisizo sahihi jambo lililochangia kutolipwa kodi ya kiasi cha Sh.8,682,521,100 (Rejea Kielelezo 71).

**Kodi ya Ongezeko la Mtaji katika Uuzwaji wa Hisa Kutoka Katika Kampuni ya VIP Kwenda PAP**

Kwa mujibu wa taarifa za TRA, kampuni ya VIP ilipaswa kulipa kodi ya mapato (income tax) badala ya Kodi ya Ongezeko la Mtaji (capital gain) kwa kuwa kampuni hiyo iliwa hisa zake zote (Kielelezo 73).

Hivyo basi, TRA iliandika barua kwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji wa VIP Bw. James Rugemalira yenyewe Kumb. Na: 3-4/100/100/223/4 ya tarehe 24 Januari, 2014 iliyosainiwa na Bw. Alfred T. Mregi kwa niaba ya Kamishna wa Walipa Kodi wakubwa, kuthibitisha kiasi cha Shilingi 38,186,584,322 kililipwa kama ‘income tax’. Pia TRA ilitoa “clearance certificate” No. IT 00393” kuoneshwa kulipwa kwa kodi na kuwezesha uuzwaji wa hisa hizo asilimia 30 kutoka kwa VIP kwenda PAP (Kielelezo 74).

**Mapendeleko**

- i. Kutokana na taarifa ya TRA kuhusu kodi ambayo haikulipwa kuhusiana na mauzo ya hisa kutoka Mechmar kwenda Piper Link, na

Piper Link kwenda PAP, inapendekezwa kwamba TRA waendelee kufuatilia kodi kutokana na mauzo ya hisa hizo.

- ii. Vyombo vyta kiuchunguzi vifanye uchunguzi wa uhalali wa miamala ya mauzo ya hisa kutoka Mechmar kwenda Piper Link, na Piper Link kwenda PAP.

## 2.5. HADIDU REJEA NA.6

Kuchunguza kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali Alisamehe Kodi ya VAT ya Jumla ya Shilingi 26 Bilioni kutokana na Tozo ya “capacity charges”, Ikiwa ni Pamoja na Usahihi wa Mamlaka yake Kisheria

### 2.5.1 Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)

#### (i) Kodi ya VAT katika Akaunti ya Escrow

Kwa mujibu wa Kipengele Na.3 cha Mkataba wa Kununua Umeme (PPA) wa mwaka 1995 baina ya TANESCO na kampuni ya IPTL; TANESCO inawajibu wa kulipa gharama za umeme (energy charges) kila itumiapo umeme na tozo ya uwekezaji (capacity charges) kila mwezi ili kufidia gharama za uwekezaji wa mitambo ya IPTL.

Tarehe 24 Septemba 2003 Bw. P.F Tarimo kwa niaba ya Kamishna wa Walipa Kodi Wakubwa wa TRA, alimwandikia barua Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO yeny Kumb. Na. 30-4/TIN100-183-471/4 akieleza kuwa TANESCO haipaswi kulipa kodi ya Ongezeko la Thamanikwa kuwa “capacity charges” haitozwi katika usambazaji, hivyo haipo kwenye wigo wa VAT. Kwa Barua hiyo, TANESCO ilitakiwa kutolipa VAT inayotokana na “capacity charges” (**Kielelezo 75**).

Hata hivyo tarehe 19 Oktoba, 2007 kupitia barua yeny Kumb. Na. 30-4/100-337-460-225 Bi. N.G.F Mrema, kwa niaba ya Kamishna wa Walipa Kodi Wakubwa wa TRA, alimwandikia Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO akiitaka TANESCO kuanza tena kulipa VAT kwenye “capacity charges” kwa madai kuwa “capacity charge” inayolipwa na TANESCO kwa makampuni mbalimbali inapaswa kutozwa kodi ya VAT kwa mujibu wa Kifungu Na.5(4) cha Sheria ya VAT ya 2006. Hivyo kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2007 TANESCO ilitakiwa kuanza kulipa tena VAT (**Kielelezo 76**).

Kuanzia mwezi Juni 2004, TANESCO ilianza kugomea tozo ya gharama za uwekezaji kwa madai kwamba mtaji wa wanahisa (equity) uliotumika kukokotolea gharama hizo haukuwa sahihi. Hata baada ya kugomea gharama za uwekezaji tangu mwezi Juni 2004, TANESCO iliendelea kuilipa IPTL gharama hizo hadi kufikia tarehe 05 Juni, 2006 (**Kielelezo 77 hadi 78 na Rejea Kielelezo 4**). Kuanzia Julai 2006 TANESCO iliweka fedha za malipoya ‘capacity charges’ kwenye akaunti ya Escrow iliyofunguliwa tarehe 05 Julai, 2006 (**Kielelezo 79**).

Baada ya kupitia Ankara za madai ya ‘capacity charges’ za IPTL kwa TANESCO na kisha kufanya mahojiano na Kaimu Mwanasheria Mkuu wa TANESCO Bw. Godson Makia na Kaimu Mkurugenzi wa Fedha wa TANESCO, ilithibitika kuwa malipo ya gharama za uwekezaji (capacity charges) yaliyofanywa kwenye akaunti ya Escrow yalijumuisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Ankara zote za madai zilizokuwa zinawasilishwa TANESCO kutoka IPTL mpaka Ankara ya mwezi Agosti,

2013 yenye Kumb.Na. 25/2013/IPTL ziliainishakodi ya VAT katika tozo za gharama ya uwekezaji (**Kielelezo 80 na 81**).

Kwa kuwa gharama za uwekezaji pamoja na VAT zililipwa kwa IPTL, wajibu wa kuwasilisha kodi hiyo katika Mamlaka ya Mapato Tanzania ulikuwa ni wa IPTL kwa mujibu wa vifungu Na. 3 na 4 vya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Mwaka 1997 (Iliyorejewa 2006). Aidha kwa kuwa TANESCO ilipinga kiwango chote kilichokuwa kinatozwa kwenye ankara husika na kwa kuwa fedha hizo ziliwekwa kwenye akaunti ya Escrow, hivyo fedha katika akaunti za Escrow zilijumuisha VAT (**Rejea Kielelezo 80 na Kielelezo 77 hadi 78**).

Kwa mujibu wa mchanganuo wa malipo ya gharama za uwekezaji toka TANESCO, hadi kufikia Mwezi Novemba, 2013 (ambapo fedha zilitolewa) akaunti ya escrow ilikuwa na jumla ya shilingi 23,460,056,122.93 kama VAT (**Kielelezo 82**).

Aliyekuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Bw. Harry Kitilya kupitia barua yenye Kumb. Na. 100-221-969/214 ya tarehe 29 Oktoba, 2013 kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha Dr.Servacius Likwelile, na nakala kwa Gavana wa Benki Kuu Prof. Benno Ndulu, alianisha kiasi cha jumla ya shilingi 26,946,487,420.80 cha VAT kilichokadiriwa kuwepo kwenye Akaunti ya Escrow hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2013 (**Kielelezo 83**).

Hata hivyo, timu ya ukaguzi baada ya kufanya ukokotoaji kulingana na nyaraka hizo, imebainika kuwa kiasi kilichopaswa kuwepo kwenye Akaunti ya Escrow kama VAT ni jumla ya shilingi 23,154,003,077(**Kiambatanisho Na.2**).Tofauti ya kiasi cha Sh.306,053,046 kati ya kiwango cha kodi kilichokokotolewa na TANESCO na kilichobainika wakati wa ukaguzi kilitokana na TANESCO kujumuisha riba iliyokuwa katika akaunti ya USD.

#### **(ii) Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)**

Katika mahojiano na Kamishna Mkuu wa TRA Bw. Rished Bade tarehe 12 Agosti, 2014 ilifahamika kuwa, TRA ilifanya jitihada za kukusanya kodi ya VAT iliyokuwepo kwenye akaunti ya Escrow kufuatia taarifa kuwa mgogoro wa gharama za uwekezaji (capacity charges) baina ya TANESCO na IPTL umekwisha na taratibu za kuhamisha fedha kutoka kwenye akaunti hiyo zimeanza (**Kielelezo 84**).

TRA kupitia barua Na. 30-4/100-184-990 ya tarehe 19 Septemba 2012 iliyosainiwa na Bw. Herbert Kabyemela kwa niaba ya Kamishna wa Walipa Kodi Wakubwa kwenda RITA, ilieleza kuhusu madai yake ya kodi ya VAT na kwamba hadi kufikia tarehe 19 Septemba 2012 kodi hiyo ilifikia kiasi cha Sh.127,315,469,878.92 (**Kielelezo 85**).

Tarehe 4 Februari, 2014 TRA ilimuandikia tena Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Dr. Servacius Likwelile barua Kumb. Na. TRA/CG/L.3ikiendelea kuiomba Wizara ya Fedha kuisaidia kukusanya kodi ya VATkutoka akaunti ya Escrow(**Kielelezo 86**). Hata hivyo barua hioiliwasilishwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha wakati fedha katika akaunti ya Escrow zimeshaanza kulipwa kwa PAP. Vilevile barua hiyo ilieleza kuwa kiasi cha VAT kwenye akaunti ya Escrow ni shilingi 21,713,935,720.75 ambacho kinatofautiana na kiasi cha Sh. 26,946,487,420.80 kilichodaiwa kuitia barua yenye Kumb. Na. 100-221-969/214 ya tarehe 29 Oktoba 2013(**Rejea Kielelezo 83**).

Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuitia barua Kumb. Na. AGCC/E.080/6/70 ya tarehe 18 Novemba, 2013 alimfahamisha Gavana wa Benki Kuu Prof. Benno Ndulu kuwa hakukuwa na kodi ya VAT katika fedha zilizokuwepo kwenye akaunti ya Escrow hivyo kutokuwepokwa kodi iliyopaswa kukusanya (**Kielelezo 87**).

Hata hivyo, katika mahojiano tuliyofanya na Kamishna Mkuu wa Kodi, alithibitisha kuwa TRA wanaendelea na hatua za kuikusanya kodi husikakutoka IPTL (**Rejea Kielelezo 84 na 87**).

#### **Mapendeleko**

Serikali kuitia TRA ihakikishe inakusanya kodi ya VAT iliyolipwa katika tozo za ‘capacity charges’ katika akaunti ya escrow ambayo haikukusanya.

## 2.6 HADIDU YA REJEA NA.7

Kuchunguza kiwango cha fedha kilicho kuwepo kwenye akaunti maalum ya BOT ‘Escrow Account’ wakati BOT inahamisha fedha zilizokuwepo katika akaunti hiyo kwenda IPTL, kiwango cha fedha kilichopaswa kuwemo katika akaunti hiyo maalum ya BOT pamoja na kiwango cha fedha kinachopaswa kulipwa zaidi kutoka TANESCO. Hii itahusisha pia kuchunguza na kutoa taarifa kuhusu kiasi cha fedha kilichowekwa na kila mhusika hadi uamuzi wa Mahakama Kuu ya Tanzania kuhusu kesi ulipotolewa

### 2.6.1 Kiasi kilichokuwepo katika akaunti ya Escrow Sh. 167,251,892,330 na USD 22,198,544

Baada ya kuhakiki taarifa ya Akaunti ya Escrow ukaguzi ulibaini kuwa hadi tarehe 15 Novemba, 2013 akaunti hiyo ilikuwa na kiasi cha Shilingi 8,020,522,330 na Dola za Kimarekani 22,198,544 (**Kielelezo 88**). Ukaguzi pia umebaini kuwa akaunti hii ilikuwa na kiasi cha Shilingi 159,231,370,000 kilicho jumuisha fedha zilizowekezwa kwenye hati fungani Shilingi 148,071,081,052 zenyeye riba ya Shilingi 11,160,288,948(**Kielelezo 89**).

**Jedwali T8: Mchanganuo wa kiasi cha fedha zilizokuwepo kwenye akaunti ya Escrow Sh.167,251,892,330 na USD 22,198,544**

Maelezo	Kiasi Kilichowekezwa (Sh)	Thamani (Sh.)	Kiasi (US \$)
<b>Hati fungani</b>			
158742	1,664,546,686	1,780,340,000	
159192	49,999,568,013	53,642,310,000	
159705	4,139,147,875	4,466,430,000	
159543	37,763,593,370	40,730,000,000	
159365	53,000,508,023	57,003,830,000	
158486	1,503,717,085	1,608,460,000	
<b>Jumla (A)</b>	<b>148,071,081,052</b>	<b>159,231,370,000</b>	
Salio katika akaunti (B)		8,020,522,330	22,198,544
<b>Jumla katika akaunti (A) + (B)</b>		<b>167,251,892,330</b>	<b>22,198,544</b>

Kufuatia maelezo ya Bw. Harbinder Singh Sethi Mwenyekiti Mtendaji wa IPTL katika barua yake ya tarehe 28 Novemba 2013, Benki Kuu ilifanya malipo ya kiasi tajwa hapo juu kwa Kampuni ya PAP kupitia akaunti Na. 9120000125324 ya dola za kimarekani na akaunti Na. 9120000125294 ya Shilingi za kitanzania katika Benki ya Stanbic (**Rejea Kielelezo 25 hadi 27**) kama ifuatavyo:

#### **Jedwali T9: Mchanganuo wa Malipo ya fedha za Escrow kwa PAP**

Tarehe	Maelezo	Kiasi (Sh.)	Kiasi (US \$)
28/11/2013	Fedha taslimu	8,020,522,330	22,198,544
10/12/2013	Sehemu ya fedha iliyotokana na hati fungani Na. 158486 ya shs.1,608,460,000 iliyopokelewa na Benki Kuu tarehe 28/11/2013.	1,447,614,000	
16/12/2013	Sehemu ya fedha iliyotokana na hati fungani Na. 158486 ya shs.1,608,460,000 iliyopokelewa na Benki Kuu tarehe 28/11/2013.	150,371,708	
24/12/2013	Sehemu ya fedha iliyotokana na hati fungani Na. 158486 ya shs.1,608,460,000 iliyopokelewa na Benki Kuu tarehe 28/11/2013.	10,474,292	
5/12/2013	Uhamisho wa kiasi kilichosalia cha hati fungani (Kwa thamani ya Bei)	157,622,910,000	
<b>Jumla</b>		<b>167,251,892,330</b>	<b>22,198,544</b>

(Kielelezo 90 na Rejea Kielelezo 88).

#### **2.6.2 Kiasi kilichotakiwa kuwepo kwenye Akaunti ya Escrow**

TANESCO ilianza kupinga ankara za IPTL kuanzia Mei 2004 hadi Agosti 2013 kulingana na notisi ya kupinga ankara za madai (Invoice Dispute Notice) iliyotolewa tarehe 17 Juni, 2004 na notisi ya mwisho ya tarehe 10 Septemba, 2013 kwa ankara ya Agosti 2013 (**Rejea Kielelezo 4 na 77 hadi 78**).

Licha ya kutoa notisi za kupinga ankara za IPTL tangu tarehe 17 Juni, 2004, TANESCO iliendelea kulipa ankara hizo hadi kufikia tarehe 05 Juni

2007 zenye jumla ya Sh. 118,291,827,820 (**Kielelezo 91 na Rejea Kielelezo 78**).

Baada ya kuhakiki ankara za madai na taarifa ya IPTL (Statement of Account) ya tarehe 1 Juni, 2014 zilizopatikana TANESCO, ukaguzi ulibaini kuwa akaunti ya Escrow ilipaswa kuwa na Sh.306,675,081,939 kutokana na ankara za IPTL kama inavyoonekana katika Jedwali T10.

**Jedwali T10: Kiasi ambacho kilipaswa kuwepo katika akaunti ya Escrow Sh.306,675,081,939**

Hati ya Madai (Ankara)	Kipindi	Kiasi kilichotozwa na IPTL (Sh.)
43/2006/IPTL	Novemba 2006	241,002,424
46/2006/IPTL	Desemba 2006	4,254,319,829
01/2007/IPTL	Januari 2007	4,442,943,422
05/2007/IPTL	Februari 2007	4,408,873,981
10/2007/IPTL	Machi 2007	3,674,061,651
14/2007/IPTL	April 2007	3,674,061,651
18/2007/IPTL	Mei 2007	3,673,311,234
20/2007/IPTL	Juni 2007	3,673,311,234
25/2007/IPTL	Julai 2007	3,627,227,707
29/2007/IPTL	Agosti 2007	3,630,392,774
32/2007/IPTL	Septemba 2007	3,630,392,774
35/2007/IPTL	Oktoba 2007	3,630,392,774
38/2007/IPTL	Novemba 2007	3,621,761,814
40/2007/IPTL	Desemba 2007	3,621,761,814
01/2008/IPTL	Januari 2008	3,365,633,718
04/2008/IPTL	Februari 2008	3,271,393,246
06/2008/IPTL	Machi 2008	3,271,393,246
09/2008/IPTL	April 08	3,271,393,246
12/2008/IPTL	Mei 2008	3,268,788,993
14-R/2008/IPTL	Juni 2008	3,268,788,993
16/2008/IPTL	Julai 2008	3,268,320,405
17/2008/IPTL	Agosti 2008	3,275,077,468
19/2008/IPTL	Septemba 2008	3,275,077,468
21/2008/IPTL	Oktoba 2008	3,275,077,468
23/2008/IPTL	Novemba 2008	3,931,891,002
25/2008/IPTL	Desemba 2008	3,931,891,002
01/2009/IPTL	Januari 2009	3,996,555,464
03/2009/IPTL	Februari 2009	3,910,184,311
04/2009/IPTL	Machi 2009	3,910,184,311
05/2009/IPTL	April 2009	3,910,184,311
06/2009/IPTL	Mei 2009	3,909,331,217
08/2009/IPTL	Juni 2009	3,909,331,217
09/2009/IPTL	Julai 2009	4,214,487,591
10/2009/IPTL	Agosti 2009	4,231,619,898
12/2009/IPTL	Septemba 2009	4,231,619,897
14/2009/IPTL	Oktoba 2009	4,231,619,897

15/2009/IPTL	Novemba 2009	2,918,946,515
17/2009/IPTL	Desemba 2009	2,918,946,515
1/2010/IPTL	Januari 2010	2,885,903,759
6/2010/IPTL	Februari 2010	2,885,903,759
8/2010/IPTL	Machi 2010	2,816,430,635
10/2010/IPTL	Aprili 2010	2,816,430,635
12/2010/IPTL	Mei 2010	2,365,353,196
15/2010/IPTL	Juni 2010	3,378,075,707
18/2010/IPTL	Julai 2010	3,483,592,409
21/2010/IPTL	Agosti 2010	3,483,592,409
23/2010/IPTL	Septemba 2010	3,483,592,409
25/2010/IPTL	Oktoba 2010	3,483,592,409
27/2010/IPTL	Novemba 2010	3,483,592,409
29/2010/IPTL	Desemba 2010	3,483,592,409
01/2011/IPTL	Januari 2011	3,877,491,133
03/2011/IPTL	Februari 2011	3,874,200,590
05/2011/IPTL-R	Machi 2011	3,874,200,590
07/2011/IPTL	Aprili 2011	3,874,200,590
10/2011/IPTL	Mei 2011	3,874,200,590
12/2011/IPTL	Juni 2011	3,874,200,590
15/2011/IPTL	Julai 2011	4,021,838,423
17/2011/IPTL	Agosti 2011	4,021,838,423
19/2011/IPTL	Septemba 2011	4,021,838,423
21/2011/IPTL	Oktoba 2011	4,021,838,423
23/2011/IPTL	Novemba 2011	4,021,838,423
25/2011/IPTL	Desemba 2011	4,021,838,423
01/2012/IPTL	Januari 2012	4,262,901,921
03/2012/IPTL	Februari 2012	4,240,469,026
05/2012/IPTL	Machi 2012	4,240,469,026
07/2012/IPTL	Aprili 2012	4,240,469,026
09/2012/IPTL	Mei 2012	4,240,469,026
11/2012/IPTL	Juni 2012	4,240,469,026
13/2012/IPTL	Julai 2012	4,218,502,728
15/2012/IPTL	Agosti 2012	4,218,502,728
17/2012/IPTL	Septemba 2012	4,218,502,728
19/2012/IPTL	Oktoba 2012	4,218,502,728
20/2012/IPTL	Novemba 2012	4,218,502,728
22/2012/IPTL	Desemba 2012	4,218,502,728
03/2013/IPTL	Januari 2013	4,197,896,910
06/2013/IPTL	Februari 2013	4,197,896,910
09/2013/IPTL	Machi 2013	4,197,896,910
12/2013/IPTL	Aprili 2013	4,197,896,910
15/2013/IPTL	Mei 2013	4,197,896,910
18/2013/IPTL	Juni 2013	4,197,896,910
21/2013/IPTL	Julai 2013	4,255,353,906
25/2013/IPTL	Agosti 2013	4,255,353,906
<b>Jumla Kuu</b>		<b>306,675,081,939</b>

(Kielelezo 92 na Rejea Kielelezo 81).

### 2.6.3 Kiasi ambacho kiliwekwa katika akaunti ya Escrow

Baada ya kufanya uhakiki wa taarifa zilizopatikana TANESCO, Wizara ya Nishati na Madini na Benki Kuu; timu ya ukaguzi ilibaini kuwa TANESCO pamoja na Wizara waliweka kwenye akaunti ya Escrow kiasi cha jumla ya Sh.182,771,388,687. Katika fedha hizo, TANESCO iliweka kiasi cha Sh. 142,008,357,587na Wizara iliweka kiasi cha Sh.40,763,031,100(**Jedwali T11**).

Wizara ilikuwa ikiwasilisha TANESCO kiasi cha Sh. 1,500,000,000 kwa kila ankara ya gharama za uwekezaji iliyotozwa na IPTL mpaka kufikia tarehe 12 Machi, 2012. Baada ya muda huo ilikuwa inaweka fedha moja kwa moja katika akaunti ya Escrow, ambapo wakati huo TANESCO haikuwa ikiweka fedha hizo hadi zilipotolewa na kulipwa kwa PAP (**Jedwali T11**).

**Jedwali T11: Fedha ambazo ziliwekwa katika akaunti ya Escrow  
Shilingi 182,771,388,687**

Tarehe	Hundi/Kumb. Ya Malipo	Kiasi (Sh.)
<b>Kiasi kilichowekwa na TANESCO</b>		
21/9/2006	Kiasi cha Awali USD 22,109,878 @ 1630	36,039,101,433
26/10/2007	TT Hundi Na. PRC/213108 NBC	4,500,000,000
18/12/2007	Hundi Na.289647 CRDB	1,500,000,000
2/1/2008	Taarifa ya Benki	1,500,000,000
14/01/2008	Hundi Na.289648 CRDB	1,500,000,000
5/2/2008	Hundi Na.289656 CRDB	1,500,000,000
7/2/2008	Hundi Na.000023 CITIBANK	23,887,100,000
17/03/2008	Hundi Na.289672 CRDB	1,500,000,000
14/04/2008	Hundi Na.289679 CRDB	1,500,000,000
14/04/2008	Hundi Na.289680 CRDB	3,797,120,604
14/05/2008	Hundi Na.984572 CITIBANK	3,405,276,892
17/6/2008	Malipo Na.69806W2HU5 CITIBANK	3,737,509,100
15/07/2008	Malipo Na.97807211YB CITIBANK	3,298,677,243

13/08/2008	Malipo Na.26807849DN CITIBANK	3,271,777,240
14/08/2008	'Electronic Banking' CITIBANK	3,271,102,859
18/09/2008	Malipo Na. 61807F5G4C 'Electronic Banking' CITIBANK	3,279,593,455
29/9/2008	Hundi Na.572369 CRDB	6,231,417,906
17/11/2008	Malipo Na. 12807QE1HF 'Electronic Banking' CITIBANK	3,277,539,665
25/3/2009	TISS Hundi Na.000057 TISS Stanbic	4,612,568,800
12/5/2009	TISS Hundi Na.PRC 21863 NBC	3,110,538,000
4/6/2009	TISS Hundi Na.PRC218936 NBC	4,253,609,000
2/10/2009	Hundi Na.000084 Stanbic	7,294,783,950
6/11/2009	TT Hundi Na.PRC219303 NBC	4,065,413,950
17/12/2009	Hundi Na.657610 CRDB	8,175,227,490
10/8/2010	Hundi Na.PRC/220782 NBC	3,500,000,000
<b>Jumla Ndogo (A)</b>		<b>142,008,357,587</b>
<b>Kiasi kilichowekwa na Wizara</b>		
12-03-2012	TISS Na.58DI11003071	9,000,000,000
18/4/2012	Hundi Na.065133 ya tarehe 2/4/12	3,000,000,000
14/05/2012	TISS Na.58DI11003804	3,000,000,000
06-05-2012	TISS Na.58DI11004125	263,031,100
06-12-2012	TISS Na.58DI11004233	1,500,000,000
22/06/2012	TISS Na.58DI11004716	1,500,000,000
16/08/2012	TISS Na.58DI12000122	1,500,000,000
17/9/2012	TISS Na.50000942	1,500,000,000
3/12/2012	TISS Na.50021314	3,000,000,000
29/1/2013	TISS Na.50042121	1,500,000,000

28/2/2013	TISS Na.50056230	1,500,000,000
25/3/2013	TISS Na.50068220	1,500,000,000
22/4/2013	TISS Na.50078784	1,500,000,000
3/5/2013	TISS Na.50083385	1,500,000,000
26/6/2013	TISS Na.50113521	3,000,000,000
24/7/2013	TISS Na.50126931	1,500,000,000
21/8/2013	TISS Na.50134695	1,500,000,000
18/9/2013	TISS Na.50143773	1,500,000,000
17/10/2013	TISS Na.50155493	1,500,000,000
<b>Jumla Ndogo (B)</b>		<b>40,763,031,100</b>
<b>Jumla Kuu (A+B)</b>		<b>182,771,388,687</b>

(Kielelezo 93 hadi 96 na Rejea Kielelelezo 79 na Kielelezo 82).

Kwa mujibu wa ankara zilizotolewa na IPTL kwa kipindi cha mgogoro, TANESCO ilipaswa kuweka kiasi cha Sh.123,903,693,252 zaidi ya fedha ilizoziweka katika Akaunti ya Escrow ikiwa ni tofauti kati ya kiasi ilichotakiwa kuweka cha Sh.306,675,081,939 (Jedwali T10) na kiasi kilichowekwa cha Sh. 182,771,388,687 (Jedwali T11).

Kiasi kilichokuwemo kwenye akaunti ya Escrow kinazidi kiasi kilichowekwa kwa takribani Shs.11,160,288,948 kutokana na riba iliyopatikana kutokana na uwekezaji wa fedha hizo katika hati fungani.

## 2.7. HADIDU REJEA NA.8

Kuchunguza Madai ya SCBHK na Wadai Wengine Yanayohusiana na Mkataba wa Ununuzi wa Umeme kati ya IPTL na Kama Serikali Ilijihadhari na Madai Mengine Yanayoweza Kutokea

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kampuni ya IPTL imekuwa ikidaiwa na wadai mbalimbali wa ndani na nje ya nchi. Tarehe 16 Machi 2012, Mahakama Kuu ya Tanzania chini ya Mh.Jaji Kajage ilitoa uamuzi kwamba kampuni ya IPTL iendelee na ufilisi kamili na kumteuwa aliyekuwa mfilisi wa muda wa IPTL, Bw. Phillip Saliboko Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA kuwa mfilisi kamili (**Kielelezo 97**).

Kufuatia uamuzi huo, Bw. Saliboko alitoa notisi kupitia magazeti mbalimbali kati ya tarehe 3-5 Aprili, 2012 iliyowataka wadai wote wa IPTL kuwasilisha madai na taarifa zao kwake kabla ya tarehe 24 Aprili, 2012 ili kufanikisha zoezi la ufilisi lililotokana na amri tajwa ya Mahakama Kuu ya Tanzania(**Kielelezo 98**).

Ilibainika kuwa jumla ya wadai wanne (4) ndiyo waliojitekeza na kuainisha madai yao ya jumla ya Sh. 321,041,365,000, USD.145,628,784.43 na GBP 1,439,836.50 (**Jedwali T2**).

**Jedwali T2: Orodha ya Wadeni Waliojitekeza**

Na.	Mdai	Maelezo ya deni	Kiasi (Sh/USD/GBP)
1	SCB-HK Limited	Mkopo uliochukuliwa chini ya Mkataba wa kukopa wa tarehe 28 Juni, 1997	USD.125,970,570.57
2	TANESCO	Tozo za gharama ya juu isivyostahili	Shs.321,041,365,000
3	Watsila Tanzania Ltd	Mkataba wa uendeshaji na ukarabati	USD.7,730,018.16
4	Watsila Netherlands B.V	Mkataba wa ujenzi	USD.11,908,195.70 GBP. 1,439,836.50

### 2.7.1 Madai ya Standard Chartered Bank Hong Kong (SCBHK)

#### i. Historia ya Mkopo wa IPTL

Baada ya kuingiwa kwa Mkataba wa Kununua Umeme (PPA) baina ya TANESCO na IPTL; Kampuni ya IPTL iliingia mkataba na Umoja

wa Mabenki ya Malaysia (Consortium of Malaysian Banks) tarehe 28 Juni 1997kwa ajili ya mkopo wa jumla ya kiasi cha Dola za Kimarekani 105,000,000 ili kuwezesha ujenzi wa mradi wa ufuaji wa umeme uliopo Tegeta. Mabenki hayo ni Sime Bank Berhad (kiasi cha Dola za Kimarekani 10,000,000), BBMB International Bank Ltd (kiasi cha Dola za Kimarekani 55,000,000), na Sime International Bank (kiasi cha Dola za Kimarekani 40,000,000) (Kielelezo 99).

Jumla ya kiasi cha USD 85,862,022 kati ya USD 105,000,000 ndicho pekee kilichopokelewa na IPTL kati ya mwezi Agosti 1997 na Desemba 1999. Mchanganuo wa mapokezi ya fedha hizo ni kama ilivyo katika **Jedwali T3:**

**Jedwali T3: Mkopo Uliotolewa na Mabenki kwa IPTL Kuanzia Mwaka 1997 hadi 1999**

Tarehe ya Mapokezi Fedha	BBMB International Bank Ltd	Sime Internationa lBank	Sime Bank Berhad	Danaharta (\$)	RHB Bank Berhad	Kiasi (\$)
Agost 20,1997	10,738,095.24	7,809,523.81	1,952,380.95			20,500,000
Sept 22,1997	4,452,380.95	3,238,095.24	809,523.81			8,500,000
Nov 03,1997	12,309,523.81	8,952,380.95	2,238,095.24			23,500,000
Nov 21,1997	261,904.76	190,476.19	47,616.05			500,000
Des 22,1997	6,547,619.05	4,761,904.76	1,190,476.19			12,500,000
Feb 20,1998	7,857,142.86	5,714,285.71	1,428,571.43			15,000,000
Machi 03,1998	523,809.52	380,952.38	95,238.10			1,000,000
Okt 16,1998	1,309,523.81	952,380.96	238,095.23			2,500,000
Des 19,1999				1,684,686.6	177,355.4	1,862,022
<b>Jumla ya Fedha</b>						<b>85,862,022</b>

(Kielelezo 100).

Madai ya SCBHK jumla ya USD 125,970,570.67 yaliwasilishwa kwa Mfilisi tarehe 24 Aprili, 2012 na Bw. Joseph Casson kwa niaba ya SCBHK (Kielelezo 101).

**ii. Mvutano Juu ya Madai ya SCB HK**

Kumekuwepo na taarifa za kupinga madai ya SCBHK kuwa mdai halali, ikielezwa kuwa matakwa ya Kifungu Na. 79(1) na Kifungu Na. 172 vya

Sheria ya Makampuni CAP 212 (iliyorekebishwa mwaka 2002) hayakutimizwa. Kifungu cha 79(1) cha Sheria hiyo kinaeleza kuwa makubaliano yeote yanayoingiwa na kampuni iliyosajiliwa Tanzania yanayogusa maslahi katika mali na biashara zake, yanatakiwa yawasilishwe pamoja na nyaraka zinazoshuhudia kwa Msajili wa Makampuni hapa nchini ndani ya siku 42 baada ya tarehe ya makubaliano hayo. IPTL haikufanya hivyo kuhusiana na deni hili na dhamana zake.

Katika Shauri na. ARB/10/20 lililofunguliwa ICSID, kifungu cha 79(1) kilijadiliwa ambapo ilielezwa kuwa kutosajiliwa kwa makubaliano yenye maslahi ya dhamana ‘security interest’ haiondoi uhalali wa deni dhidi ya kampuni husika (ICSID ARB/10/20, Aya 169, Ukurasa 44) (**Kielelezo 102**).

Ilibainika pia kuwa IPTL ilikuwa ikifanya marejesho hata baada ya deni kununuliwa na SCBHK. Kwa maelezo ya SCBHK katika kipindi cha Novemba 2005 mpaka Aprili 2007, IPTL ilikuwa ikifanya malipo moja kwa moja kwa SCBHK. Hili linathibitika katika barua ya IPTL Na. IPTL/2014-002 ya 03 Februari, 2014 kwenda kwa Waziri wa Nishati na Madini Prof. Sospeter Muhongo, iliyosainiwa na Dr. Magesveran Subramaniam Mkurugenzi wa Uendeshaji na Bw. Joseph Makandege Mwanasheria wa IPTL, ilieleza kwamba hadi kufikia mwaka 2007 IPTL ilikwishalipa jumla ya kiasi cha Dola za Kimarekani 58.69 milioni, ambapo kati ya hizo Dola za Kimarekani 20 milioni zililipwa kwa SCBHK (**Kielelezo 103**).

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mh. Jaji Frederick Werema pamoja na mambo mengine kuitia barua Na AGCC/E.80/6/65 ya tarehe 2 Oktoba, 2013 kwenda kwa Katibu Mkuu Hazina Dr. Servacius Likwelile akizungumzia deni la SCBHK alibainisha kuwa madai ya SCBHK hayana athari yoyote kwa Serikali baada ya uamuzi wa kuhamisha fedha kutoka kwenye akaunti ya Escrow kwenda IPTL, kwa msingi kwamba IPTL ni Kampuni iliyobaki kuwa hai. Hivyo SCB HK wanaweza kuendelea na madai yake kwa IPTL kama wadeni wengine (**Rejea Kielelezo 20**).

Baada ya kuhakiki nyaraka za deni la SCB Hong Kong nchini China tarehe 14 Septemba, 2014 ilibainika kuwa SCB HK ilinunua deni hilo mwezi Agosti 2005. Hati halisi ya hisa saba (7) za Mechmar ambazo pia zilitumiwa kama dhamana ya mkopo ziliwasilishwa na kuhakikiwa (**Kielelezo 104**).

### 2.7.2 Madai ya TANESCO

Katika vipindi tofauti mwaka 2008, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dr. Idrisa Rashid alifanya mawasiliano mbalimbali na IPTL kuhusiana na madai ya TANESCO kwa IPTL yaliyotokana na kutozwa zaidi kiwango cha tozo ya uwekezaji (capacity charges). Kupitia barua yake Na. MD/IPTL ya tarehe 12 Mei, 2008 kwenda kwa Bw. C. Parthiban Meneja

Mkuu IPTL alibainisha kuwa TANESCO inapaswa kurejeshewa kiasi cha fedha kilicholipwa zaidi isivyostahili kwa IPTL (**Kielelezo 105**).

Barua za tarehe 4 Juni, 2008 na tarehe 16 Juni, 2008 zenye Kumb. Na. MD/IPTL kutoka kwa Dr. Idrisa Rashid kwenda kwa aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa IPTL, Bw. Datuk Baharuden Majid zilieleza kuwa hadi kufikia Machi, 2008 TANESCO ilikwisha lipa tozo ya uwekezaji zaidi ya kiwango kilichotakiwa kulipwa kwa kiasi cha Shilingi 157 Bilioni (Sh. Bilioni 195.7 ikiwa ni pamoja na riba)(**Kielelezo 106 na 107**).

Madai ya TANESCO yaliwasilishwa kwa mfilisi wa muda kupitia kiapo cha tarehe 16 Aprili, 2012 na aliyekuwa Mwanasheria wa TANESCO Bw. Godwin Simba Ngwilimi juu ya deni la TANESCO la jumla ya Shilingi 321,041,364,000dhidi ya IPTL kuhusiana na gharama za uwekezaji zilizotozwa zaidi (overstated capacity payments) kwa TANESCO. Katika kiapo hicho Bw. Ngwilimi alieleza juu ya msingi wa deni hilo la TANESCO (**Kielelezo 108 na 109**). Ilabainishwa kupitia kiapo hicho kwamba katika kipindi cha kuanzia Januari 2002 hadi Novemba 2006 malipo ya tozo ya gharama ya uwekezaji yalilipwa kwa kadiri ya ankara zilizowasilishwa zikijumuisha kiwango cha mrejesho wa mtaji (return on equity) cha asilimia 22.31 ya mtaji uliolipwa (paid up capital) wa USD 36.5 milioni.

Madai ya TANESCO yalijikita katika hoja ya kuwa mtaji halisi uliochangiwa na wanahisa wa IPTL (paid up share capital) ni Sh.50,000. Katika kiapo hicho ilielezwa kuwa, kwa kuwa mkopo wa wanahisa haupaswi kuwa na riba, katika kipindi cha kuanzia Januari 2002 mpaka Novemba 2006 TANESCO ililipa zaidi kiasi cha Shilingi 152,359,252,000 kwa IPTL, ambapo kati yake Shilingi 20,986,785,00 kiliwekwa katika Akaunti ya Escrow na kiasi cha Shilingi 131,372,458,000 kililipwa moja kwa moja kwa IPTL. TANESCO ilifanya malipo ya jumla ya Shilingi 84,780,308,000 katika akaunti ya Escrow katika kipindi cha kuanzia Desemba 2006 hadi Machi 2012. Mchanganuo wa deni hili ni kama ilivyo katika Jedwali T4 hapa chini:

#### Jedwali T4: Mchanganuo wa Madai ya TANESCO kwa IPTL

Na.	Maelezo	Kiasi (Sh.)
1	Kiasi kilichocholipwa Zaidi (Januari 2002 - Novemba 2006)	152,359,252,000
2	Malipo kwenda escrow (Desemba 2006 - Machi 2012)	84,780,308,000
3	Riba katika kiasi kilicholipwa Zaidi	69,541,507,000
4	Riba katika kiasi kilicholipwa escrow	14,360,297,000
	<b>Jumla</b>	<b>321,041,364,000</b>

### **Maelezo ya Bodi ya TANESCO Juu ya Madai ya Shilingi Bilioni 321**

Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO kupitia barua Na. SEC.356/Audit/82014 ya tarehe 19 Agosti, 2014 iliyosainiwa na Mwenyekiti wake Jenerali Mstaafu Robert Mboma (**Rejea Kielelezo 106**) kwenda kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilielezea kutokifahamu kiapo cha tarehe 12 Aprili, 2012 kilichotolewa na Bw. Godwin Simba Ngwilimi kwa niaba ya TANESCO kuthibitisha madai ya jumla ya Shilingi bilioni 321.

Barua hiyo ilibainisha kuwa deni la TANESCO lililotolewa kiapo halifahamiki kwa Shirika na kwamba kiapo hicho kilikuwa ni matakwa binafsi ya Bw. Godwin Ngwilimi na ushauri wa wataalam wa masuala ya fedha kutoka Castalia LLC ambao walipewa kazi hiyo na Kampuni ya Wanasheria ya Mkono& Co, na kwamba TANESCO hawakuwahi kupokea ushauri rasmi kutoka kwa Castalia LLC kuhusiana na madai hayo kabla au baada ya notisi ya Mfilisi wa Muda.

Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO alibainisha kuwa Menejimenti ya Shirika haikuidhinisha suala la Bw. Godwin S. Ngwilimi awasilishe madai yake kwa Mfilisi kwa niaba ya TANESCO. Pia ilielezwa kuwa madai haya yaliyowasilishwa dhidi ya IPTL ni madai ambayo yalikuwa tayari ndio msingi wa shauri la ICSID Na. ARB/10/20 (ICSID 2) ambalo lilikuwa bado halijaamuliwa hivyo TANESCO isingeweza kuwasilisha madai yanayohusu masuala ambayo bado hayajaamuliwa na ICSID.

Katika Shauri ICSID Na. ARB/98/8 (ICSID 1) ilikubalika kuwa uwiano wa Deni na Mtaji kuwa 70:30 ambapo kutokana na uamuzi huo gharama za mradi zilishushwa kutoka USD 163.5 Milioni kuwa 127.2 Milioni, ikiwa na maana kwamba deni lingekuwa USD 89.041 Milioni (ambayo ni 70%) na mtaji USD 38.160 Milioni (ambayo ni 30%).

Kiasi cha USD 38.160 Milioni kilipaswa kuwa ni mchango wa wanahisa (paid share capital) badala yakekiasi hichokilionyeshwa kama mkopo wa wanahisa. Katika ukokotoaji wa ‘capacity charges’ IPTL ilionesa kiasi hicho kama mchango wa wanahisa.

ICSID ilitoa uamuzi wa awali mwezi Februari 2004 (ICSID 2) uliojumuisha pamoa na mambo mengine kwamba kiwango cha tozo ya gharama za uwekezaji zinapaswa kukokotolewa upya ili kuonyesha kwamba mtaji (equity contribution) wa IPTL ultokana na mkopo wa wanahisa (shareholder loan) na siyo mtaji wa wanahisa uliolipiwa (paid up share capital) (**Rejea Kielelezo 14**).

#### **2.7.3 Madai ya Watsila Tanzania Limited na Watsila Netherlands B.V**

Madai ya kampuni ya Watsila Tanzania ya kiasi cha Dola za Kimarekani 7, 730,018.16 yaliwasilishwa kwa Mfilisi na Bw.Jaakko Kaihua katika kiapo cha tarehe 24 Aprili, 2012 (**Kielelezo 110**). Madai haya yalitokana na

gharama za Mkataba wa Uendeshaji na Ukarabati wa Mitambo Kati ya IPTL na Watsila.

Madai ya Watsila Netherlands B.V ya kiasi cha Dola za Kimarekani 11,908,195.70 naPaundi za Uingereza 1,439,836.50 yaliwasilishwa kwa Mfilisi na Anton Philip Huibert van Velzen katika kiapo cha tarehe 19 Aprili, 2012. Madai haya yalihusiana na Mkataba wa Ujenzi kati ya IPTL na Watsila Netherlands B.V (iliyokuwa Wartsila Diesel B.V) (**Kielelezo 111**).

Kwa mujibu wa mahojiano ya tarehe 18 Agosti 2014 na Mwanasheria wa IPTL Bw. Joseph Makandege, wadeni hawa wawili wanaendelea kulipwa na IPTL katika utaratibu waliokubaliana.

#### **2.7.4 Wadai waliomo katika taarifa ya Mfilisi hadi kufikia tarehe 5 Septemba, 2013**

Taarifa ya makabidhiano ya kampuni ya IPTL kutoka kwa mfilisi wa muda Bw. Phillip Saliboko kwenda kwa Pan Africa Power Solutions (T) Ltd (PAP) (**Kielelezo 112**), pamoja na mambo mengine yalijumuisha madeni ya Kampuni ya IPTL ya jumla ya Dola za Kimarekani 14,623,062.02(**Jedwali T5**). Madeni yaliyokabidhiwa ni yale ambayo mdai husika na IPTL walifikiana na kusaini kuwa ni madeni stahiki na yaliyokubalika (Uncontested Creditors). Hivyo taarifa husika haikujumuisha madeni yanayobishaniwa ambayo ni pamoja na deni la SCBHK, Watsila Tanzania, Watsila Netherlands na TANESCO (**Rejea Jedwali T2**).

##### **Jedwali T5: Wadeni waliojumuishwa katika taarifa ya makabidhiano**

Na.	Mdai	Maelezo ya deni	Kiasi USD
1	RITA	Fees for insolvency services	2,219,920.08
2	Law Associates Advocates	Legal services	4,500,000.00
3	Bulwark Associates Advocates	Legal services	3,850,000.00
4	Total Tanzania Limited	Fuel consignments	2,580,000.00
5	Nixon Peabody	Legal services	823,141.94
6	Asyla Attorneys	Legal services to PAP	500,000.00
7	MK-Employment and Labour Solutions Associates	Human Resources Consultancy Services	150,000
	<b>Jumla</b>		<b>14,623,062.02</b>

#### **2.7.5 Tahadhari Iliyochukuliwa na Serikali Dhidi ya Madai Yanayoweza Kujitokeza**

Kabla ya kutolewa kwa fedha katika akaunti ya escrow, Serikali ilichukua tahadhari dhidi ya madai mengine yanayoweza kujitokeza kuhusiana na

fedha zilizotolewa. Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Eliachim Maswi kupitia barua Na SBD.88/147/01/4 ya terehe 20 Septemba, 2013 aliyomwandikia Mkurugenzi Mtendaji wa IPTL, Bw. Harbinder Singh Sethi (**Rejea Kielelezo 16**) aliitaka IPTL kutokuwa na madai zaidi dhidi ya Serikali na TANESCO kuhusiana na akaunti ya escrow.

Kufuatia barua hiyo ya Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini; IPTL kupitia barua Na IPTL/GEN/010-2013 ya tarehe 28 Oktoba, 2013 (**Kielelezo 113**) iliwasilisha kinga yake kwa Serikali na Benki Kuu dhidi ya madai yanayoweza kujitokeza (**Rejea Kielelezo 49**). Serikali na Benki Kuu zilipewa kinga dhidi ya madai ya sasa na ya baadaye yanayoweza kujitokeza baada ya kutolewa fedha za Escrow, na kwamba endapo kutatokea madai au mashitaka kuhusiana na fedha hizo IPTL itawajibika.

#### **Mapendekezo**

- i. Ni vyema SCBHK ikafuatilia ulipwaji wa deni lake kutoka IPTL ambaye ndiye mdeni wake, kwa kuwa baada ya hukumu ya tarehe 5 Septemba 2013 ya Mahakama Kuu ya Tanzania ambapo IPTL ilirejeshwa kuwa kampuni hai.
- ii. Menejimenti ya TANESCO iangalie jinsi ya kutekeleza uamuzi wa ICSID juu ya Shauri Na. ARB/10/20 (ICSID 2) ili kuwezesha majadiliano juu ya kiwango sahihi cha tozo ya gharama za uwekezaji.

## **2.8 HADIDU REJEA NA. 11**

**Kufanya Uhakiki wa Hatua Zilizofuatwa Tangu Kesi Ilipofunguliwa Hadi Uamuzi wa Mahakama Ulipotolewa. Kiasi Kilichokuwa Katika Akaunti Baada ya Uamuzi wa Mahakama Kuu na Kilivyolipwa Kulingana na Mkataba**

### **2.8.1 Utangulizi**

Katika uhakiki wa hatua zilizofuatwa hadi uamuzi wa mahakama, ieleweke kwamba ukaguzi haulengi kukosoa maamuzi ama kuingilia uhuru wa kikatiba wa mahakama, kwa kuwa suala hili haliko ndani ya majukumu na mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

### **2.8.2 Yaliyojitokeza katika Ukaguzi**

Tangu kuanza kwa Mkataba wa kuzalisha umeme (PPA) baina ya TANESCO na IPTL tarehe 26 Juni 1995, mashauri mbalimbali yalifunguliwa dhidi ya Kampuni ya IPTL, TANESCO, Benki Kuu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mahakama mbalimbali za ndani na nje ya nchi, pia katika Kituo cha Usuluhihi wa Migogoro ya Uwekezaji cha Kimataifa (ICSID). Baadhi ya mashauri yaliyofunguliwa yalihusu pande mbili za mkataba huo, migogoro ya wanahisa wa IPTL na migogoro ya wadeni wa IPTL kama ifuatavyo:

- i. Misc Civil Cause No. 49 of 2002 kati ya VIP dhidi ya IPTL na Mechmar Corporation katika (Mahakama Kuu ya Tanzania),
- ii. Misc Civil Cause No. 254 of 2003 kati ya VIP dhidi ya IPTL, Mechmar and The Administrator General /Official Receiver katika (Mahakama Kuu ya Tanzania),
- iii. Civil Application No.163 of 2004 kati ya VIP dhidi ya Mechmar katika Mahakama ya Rufaa,
- iv. Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) dhidi ya Independent Power Tanzania Limited - ICSID case No. ARB /98/8,
- v. Standard Chartered Bank dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania- ICSID Case No. ARB /10/12,
- vi. Standard Chartered Bank (Hong Kong) Limited dhidi ya Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) ICSID case No ARB/10/20,
- vii. Martha Kaveni Renju the Administrator Receiver of IPTL dhidi ya IPTL Shauri Na.124 ya 2003,
- viii. Martha Kaveni Renju the Administrator Receiver of IPTL dhidi ya IPTL na VIP Engineering and Marketing ltd Shauri Na.98 la 2013,
- ix. Shauri la Mapitio Na.1 la 2012 kati ya Standard Chartered Bank (hong Kong) dhidi ya Mechmar Corporation, VIP Engineering and Marketing, IPTL, The Liquidator of IPTL, The Bank of Tanzania, TANESCO na TRA katika Mahakama ya Rufaa ya Tanzania.

Pamoja na kwamba mashauri mengi yalifunguliwa, ukaguzi huu maalum ulijikita katika shauri Na. 49 ya 2002 na Na. 254 ya 2003 kati ya VIP dhidi ya IPTL, Mechmar Corporation na Administrator General katika Mahakama Kuu ya Tanzaniaambayo yaliamuliwa kwa pamoja.

#### **2.8.3 Consolidated Misc Civil Cause No. 49 ya 2002 na Na.254 ya 2003: VIP dhidi ya IPTL na Mechmar (Mahakama Kuu ya Tanzania)**

Shauri Na. 49 la 2002 lililohusu maombi ya ufilisi wa kampuni ya IPTL (Application for winding up) lilifunguliwa na VIP (mwanahisa 30%) dhidi ya Mechmar (mwanahisa 70%) na kampuni ya IPTL, ambapo mdai aliiomba Mahakama Kuu ya Tanzania itoe amri ya kufilisiwa kwa Kampuni ya IPTL kutokana na kutofautiana kwa wanahisa hao.

Baada ya kusikilizwa kwa shauri husika, tarehe 16 Desemba 2008 Mahakama Kuu ya Tanzania ilikubaliana na ombi la VIP na kuamuru IPTL kuwekwa katika ufilisi wa muda (Provisional Liquidation) (**Rejea Kielelezo 56**).

Katika vipindi mbalimbali kampuni ya IPTL iliwekwa katika ufilisi wa muda na ufilisi kamili, ambapo mnamo tarehe 30 Agosti 2013 VIP Engineering & Marketing kupitia Ngalo & Co advocates kwa barua Na. NCA/DSM/1332/13 baada ya kutangazwa tarehe 26 Agosti 2013, iliwasilisha Mahakama Kuu ya Tanzania ombi la kuondoa shauri la ufilisi wa IPTL. VIP aliiomba Mahakama mambo matano kama ifuatavyo:

- (i) Kuondosha ombi la ufilisi wa kampuni ya IPTL bila kutoa amri yoyote kuhusu gharama za kesi,
- (ii) Kutenguliwa kwa uteuzi wa mfilisi wa muda,
- (iii) Kwamba Mfilisi wa Muda akabidhi mali zote za IPTL, ikiwa ni pamoja na mtambo wa kuzalisha umeme kwa Pan Africa Power Solutions (T) limited ambaye amedhamiria kuwalipa wadai wote halali wa IPTL na kuongeza uwezo wa mtambo hadi kufikia MW 500 na kuza umeme kwa TANESCO kwa bei ya kati ya senti 6 hadi 8 za Dola za Kimarekani kwa uniti baada ya kuzingatia maslahi ya umma kama ilivyonukuliwa hapa chini:

*“that the provisional liquidator shall hand over all the affairs of IPTL including the IPTL Power Plant (the plant) to PAP, which has committed to pay off all legitimate Creditors of IPTL and to expand the plant capacity to about 500MW and sale power to TANESCO at a tariff of between Us cents 6 and 8 /Unit in the shortest possible time after taking over in the public interest”*

- (iv) Washirika wa kesi wanayo hiari ya kuanzisha madai mapya katika mahakama yoyote yenye mamlaka stahili dhidi ya mshirika yoyote

pale watakaposhindwa kufikia makubaliano nje ya mahakama juu ya masuala yahusuyo IPTL,

- (v) Kwamba mahakama imepokea na kutambua makubaliano baina ya VIP na PAP.

Kufuatia maombi hayo ya VIP, tarehe 5 Septemba 2013 Mahakama Kuu ya Tanzania chini ya Mh. Jaji J.H.K Utamwa ilikubali na kutoa amri ya utekelezwaji wa masuala yote matano (5) kama yalivyoombwa na VIP(**Rejea Kielelezo 7**).

Kutokana uamuzi huo wa Mahakama, Mfilisi wa Muda alikabidhimasuala yote yahusuyo kampuni ya IPTL kwa PAP (**Rejea Kielelezo 112**).

#### **2.8.4 Kiasi Kilichokuwa Katika Akaunti Baada ya Uamuzi wa Mahakama Kuu na Kilivyolipwa Kulingana na Mkataba**

Sehemu hii imetolewa taarifa katika hadidu ya rejea Na.7

##### **Mapendeleko**

Kwa kuwa PPA inahusu manunuzi ya megawati 100, katika utekelezaji wa uamuzi wa mahakama ambao unaitaka IPTL kuongeza uzalishaji wa umeme kufikia megawati 500;TANESCO na IPTL wapitie na kujadili upya mkataba husika.

## SURA YA TATU

### 3.0 HITIMISHO

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatoa shukrani za dhati kwa watu wote binafsi, vyombo mbali mbali na taasisi za Serikali na binafsi kwa ushirikiano walio tupatia katika kufanikisha zoezi la ukaguzi huu maalumu.

Francis Mwakapalila

**KAIMU MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

## **Viambatanisho**

### **Kiambatanisho Na.1**

#### **Mahojiano/Majadiliano yaliyofanyika wakati wa ukaguzi huu**

<b>Na</b>	<b>Jina</b>	<b>Nafasi</b>
1	Bw. Eliachim Maswi	Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini
2	Dr. Servacius Likwelile	Katibu Mkuu Wizara ya Fedha
3	Mh. Zito Zuberi Kabwe	Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu
4	Ms. Saada Mkuya Salum	Waziri wa Fedha
5	Prof. Benno Ndulu	Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania
6	Gen. Robert Mboma (Rtd)	Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO
7	Eng. Felschesmi Mramba	Mkurungenzi Mtendaji wa TANESCO
8	Bw. Rished Bade	Kamishina Mkuu wa TRA
9	Mh. Jaji Fredrick Werema	Mwanasheria Mkuu wa Serikali
10	Bw. Harbinder Sethi	Mwenyekiti Mtendaji wa PAP
11	Bw. James Rugemalila	Mkurugenzi wa VIP Engineering & Marketing
12	Mh. Vicent Nyerere	Mbunge
13	Mh. David Kafulila	Mbunge
14	Mh. Nimrodi Mkono	Mbunge
15	Dr. Kapanga	Wakili Mkono & Co. Advocates
16	Bw. Philip G. Saliboko	Mtendaji Mkuu RITA
17	Bw. Frank Kanyusi	Msajili wa Biashara na Leseni (BRELA)
18	Dr. Magesvaran Subramania	Aliyekuwa Mkurungenzi Uendeshaji IPTL
19	Bw. Patric Rutabanzibwa	Katibu Mkuu Mstaafu
20	Bi. Martha Renju	Msimamizi wa Hisa za IPTL wa SCB HK
21	Mh. Jaji Othman Chande	Jaji Mkuu wa Tanzania
22	Prof. Sospeter Muhongo	Waziri wa Nishati na Madini
23	Bw. Joseph Casson	Mkurugenzi Mtendaji SCB HK
24	Bw. Gasper Nyika	Wakili IMMMA (SCB HK)
25	Bw. Charles Rwechungura	Wakili CRB Africa Legal (Mechmar)
26	Bw. Cyril J. Pesha	Wakili CRB Africa Legal (Mechmar)
27	Bw. Seni Malimi	Wakili K&M Advocates
28	Bw. Joseph Makandege	Mwanasheria wa Kampuni ya IPTL
29	Bw. Godson Makia	Ag. Chief Legal Counsel and Company Secretary
30	Ms. Lina Msanga	Meneja wa Udhagini na Ufilisi RITA
31	Bw. Lim Litt	Wakili (Wafilisi wa Mechmar Malaysia)
32	Bw. Kyrean	Mshauri Mtaalam (SCB HK)
33	Bw. Ismail Mustafa	Mwanasheria wa Benki ya Tanzania

## Kiambatanisho Na.2

### VAT Kwenye Akaunti ya Escrow Sh. 23,154,003,077

Tarehe	Kiasi (Sh.)	Hundi/Kumb. ya Malipo	Kiasi cha VAT (Sh.)	KIWANGO (%)
<b>Kiasi kilichowekwa na TANESCO</b>				
21/9/2006	36,039,101,433	Kiasi cha Awali US \$ 22,109,878 @ 1630		
26/10/2007	4,500,000,000	TT Hundu Na. PRC/213108 NBC	750,000,000	20%
18/12/2007	1,500,000,000	Hundi Na.289647 CRDB	250,000,000	20%
2/1/2008	1,500,000,000	Taarifa ya Benki	250,000,000	20%
14/01/2008	1,500,000,000	Hundi Na.289648 CRDB	250,000,000	20%
5/2/2008	1,500,000,000	Hundi Na.289656 CRDB	250,000,000	20%
7/2/2008	23,887,100,000	Hundi Na.000023 CITI BANK	3,981,183,333	20%
17/03/2008	1,500,000,000	Hundi Na.289672 CRDB	250,000,000	20%
14/04/2008	1,500,000,000	Hundi Na.289679 CRDB	250,000,000	20%
14/04/2008	3,797,120,604	Hundi Na.289680 CRDB	250,000,000	20%
14/05/2008	3,405,276,892	Hundi Na.984572 CITI BANK	632,853,434	20%
17/6/2008	3,737,509,100	Malipo Na.69806W2HU5 CITI BANK	567,546,149	20%
15/07/2008	3,298,677,243	Malipo Na.97807211YB CITI BANK	622,918,183	20%
13/08/2008	3,271,777,240	Malipo Na.26807849DN CITI BANK	549,779,541	20%
14/08/2008	3,271,102,859	'Electronic Banking' CITI BANK	545,296,207	20%
18/09/2008	3,279,593,455	Malipo Na. 61807F5G4C 'Electronic Banking' CITI BANK	545,183,810	20%
29/9/2008	6,231,417,906	Hundi Na.572369 CRDB	546,598,909	20%
17/11/2008	3,277,539,665	Malipo Na. 12807QE1HF 'Electronic Banking' CITI BANK	1,038,569,651	20%
25/3/2009	4,612,568,800	TISS Hundu Na.000057 TISS Stanbic	768,761,467	20%
12/5/2009	3,110,538,000	TISS Hundu Na.PRC 21863 NBC	474,488,847	18%
4/6/2009	4,253,609,000	TISS Hundu Na. PRC218936 NBC	648,855,610	18%
2/10/2009	7,294,783,950	Hundi Na.000084	1,112,763,653	18%

		Stanbic		
6/11/2009	4,065,413,950	TT Hund Na.PRC219303 NBC	620,147,891	18%
17/12/2009	8,175,227,490	Hundi Na.657610 CRDB	1,247,068,600	18%
10/8/2010	3,500,000,000	Hundi Na.PRC/220782 NBC	533,898,305	18%
<b>Jumla Ndogo (A)</b>	<b>142,008,357,587</b>		<b>16,935,913,590</b>	
<b>Kiasi kilichowekwa na Wizara ya Nishati na Madini</b>				
12-03-2012	9,000,000,000	TISS Na.58DI11003071	1,372,881,356	18%
18/4/2012	3,000,000,000	Hundi Na.065133 ya tarehe 2/4/12	457,627,119	18%
14/05/2012	3,000,000,000	TISS Na.58DI11003804	457,627,119	18%
06-05-2012	263,031,100	TISS Na.58DI11004125	40,123,388	18%
06-12-2012	1,500,000,000	TISS Na.58DI11004233	228,813,559	18%
22/06/2012	1,500,000,000	TISS Na.58DI11004716	228,813,559	18%
16/08/2012	1,500,000,000	TISS Na.58DI12000122	228,813,559	18%
17/9/2012	1,500,000,000	TISS Na.50000942	228,813,559	18%
3/12/2012	3,000,000,000	TISS Na.50021314	457,627,119	18%
29/1/2013	1,500,000,000	TISS Na.50042121	228,813,559	18%
28/2/2013	1,500,000,000	TISS Na.50056230	228,813,559	18%
25/3/2013	1,500,000,000	TISS Na.50068220	228,813,559	18%
22/4/2013	1,500,000,000	TISS Na.50078784	228,813,559	18%
3/5/2013	1,500,000,000	TISS Na.50083385	228,813,559	18%
26/6/2013	3,000,000,000	TISS Na.50113521	457,627,119	18%
24/7/2013	1,500,000,000	TISS Na.50126931	228,813,559	18%
21/8/2013	1,500,000,000	TISS Na.50134695	228,813,559	18%
18/9/2013	1,500,000,000	TISS Na.50143773	228,813,559	18%
17/10/2013	1,500,000,000	TISS Na.50155493	228,813,559	18%
<b>Jumla Ndogo (B)</b>	<b>40,763,031,100</b>		<b>6,218,089,487</b>	
<b>Jumla Kuu (A+B)</b>	<b>182,771,388,687</b>		<b>23,154,003,077</b>	